epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Alhamisi Januari 16, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581923
MWANGA WA JAMII
LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper

## KASHFA YA RUSHWA

# Video mtandaoni zazua balaa polisi



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, SACP Jumanne Muliro, akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu kukamatwa kwa askari wa kikosi cha usalama barabarani kwa tuhuma za rushwa pamoja mganga wa kienyeji anayedaiwa kuiba watoto. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

• **Trafiki** watiwa mbaroni wakidaiwa kupokea rushwa za madereva... *ukurasa 3*

UKURASA WA 2

**W'biashara** wakoshwa maboresho Bandari Dar






**Wizara** yatoa kauli wanafunzi kurekodi video za utupu

UKURASA WA 5

UKURASA WA 5

**DED** apandishwa kizimbani mashtaka ya uhujumu uchumi



## MKUTANO NISHATI

## Serikali yataja itakayoyavuna, siri Tanzania kuwa mwenyeji

UKURASA 13

## Watoto walioibwa wakutwa mafichoni kwa sangoma

UKURASA 3

# Mnyukano wa vigogo CHADEMA waishtua LHRC, yataja dawa

UKURASA 2



Wafanyabiashara wadogo wa eneo la MR, mjini Iringa wakiwa wamefunga barabara ya MR-Mkwawa jana, wakiushinikiza uongozi wa serikali ya mkoa huo, kufika kuwasikiliza baada ya mgambo wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa kuvunja vibanda vyao na kuharibu mali. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

**MICHEZO** SERIKALI YAWAANGUKIA WADAU KUELEKEA CHAN UK.23 **KATUNI** UK.6

# Biteko: Serikali kukamilisha kuuza umeme nje ya nchi

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko, amesema Tanzania ina umeme wa ziada wa Megawati 740 na kwamba katika serikali ya awamu hii ya sita inakwenda kukamilisha mipango yake ya miaka mingi ya kuuza umeme nje ya nchi.

Dk. Biteko ambaye ni waziri mwenye dhamana ya Nishati, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kukagua maandalizi ya Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC), utakaotumika katika mkutano wa nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuanzia Januari 27 na 28 mwaka huu.

Alisema tayari maandalizi kwa ajili ya kuanza kuuza umeme huo yameanza kwa kujenga laini zitakazotumika kusafirisha umeme huo kwenda nchi jirani ikiwamo Zambia.

"Nchi yetu tunao umeme wa ziada, kwa mitambo yetu yote tuliyonayo tukijumlisha, tuna zaidi ya megawati 740 ambayo ipo tu ambayo tungeweza kuitumia kama tungekuwa na mahali pa kupeleka," alisema Dk. Biteko.

"Lakini hatuwezi kupeleka huo umeme kwa wenzetu kwa sababu hatuna njia za kuwapelekea. Kwa mfano Zambia, wana changamoto ya mgawo wa umeme kwa muda mrefu, kwa sasa tunajenga laini ya kutoka Iringa, Mbeya kwenda Tunduma, baadaye tuunganishe na wenzetu wa Zambia, na tayari tuko kwenye hatua za mwisho majadiliano ya kuwauzia umeme.

"Ile ndoto ya mliyokuwa mkiisikia kwamba tutauza umeme kwa wenzetu, imesemwa kwa miaka mingi, inakwenda kutokea kwenye awamu ya sita ya serikali.

Tayari mikakati hiyo ipo, tumeikamilisha, hivi ninavyozungumza tumeshajiunga na wenzetu wa Kenya, Burundi na Rwanda kupitia mradi wa Rusumo, wakihitaji umeme hata jana tutawapatia," alisema Dk. Biteko.

Kadhalika, alisema mwezi ujao, wakuu wa nchi hizo tatu wanaoshirikiana kwenye mradi wa Rusumo, watauzindua rasmi mradi huo.

Kuhusu mkutano huo wa wakuu wa nchi, Dk. Biteko alisema maandalizi yamekamilika kwa asilimia 95 na kwamba marais wengi pamoja na wakuu wa taasisi za kimataifa wamethibitisha kushiriki.

Alitaja sababu zilizochangia Tanzania kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa mkutano huo kuwa ni pamoja na kupiga hatua kwenye diplomasia pamoja na kwenye sekta ya nishati hususani kwa kufanikiwa kupeleka umeme vijiji 12,318 na vitongoji 64,274 na tayari vitongoji 34,000 vimekwisha kusambaziwa.

Alisema faida zitakazopatikana kutokana na uwapo wa mkutano huo ni pamoja na kuongezwa kwa kasi ya Watanzania watakaounganishwa na umeme ifikapo mwaka 2030 hadi kufikia milioni 13.5. badala ya milioni 5.2.

Faida nyingine zitakazotokana na mkutano huo ni kuongezeka kwa fursa za uwekezaji, kuimarisha biashara na kuongeza heshima ya Tanzania kimataifa.

Alisema mpaka sasa marais wengi na wakuu wa taasisi za kimataifa wamethibitisha kushiriki katika mkutano huo.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alisema mkoa huo ni mwenyeji wa mkutano huo, wamekubaliana na kikosi cha usalama barabarani kupunguza foleni barabarani na kupunguza baadhi ya usafiri ikiwamo bajaji na pikipiki.

Pia, aliwataka wenye malori ambao yanapaki pembezoni mwa barabara inayotoka uwanja wa ndege kwenda mjini, kuyaondoa haraka ifikapo Januari 20.

"Kila mwenye lori atafute eneo la kuliegesha, kwa sababu zile barabara ni lazima ziwe wazi ili kupendezesha mji wetu," alisema Chalamila.

Alisema wamejiandaa kunadi huduma mbalimbali ikiwamo za afya, mazoezi, utalii na watakuwa na maonesho ya baadhi ya bidhaa na kwamba wamepata taa 400 ambazo zitafungwa ili kusaidia kufanyika kwa biashara saa 24.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (kushoto), akizungumza na kamati ya maandalizi ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika utakaojadili nishati ya umeme utakaowakutanisha wakuu 14, wakati akikagua ukarabati wa jengo la mikutano la Mwalimu Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wafanyabiashara wakoshwa maboresho Bandari ya Dar

**Na Mwandishi Wetu**

MABORESHO ya miundombinu katika Bandari ya Dar es Salaam yamepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za kushughulikia mizigo kutoka Dola za Marekani 8,000 hadi Dola 3,000.

Khamis Livembe, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam baada ya kuzuru bandarini huko na wafanyabiashara wenzake na kuona uboreshaji wa miundombinu na utendaji wa bandari hiyo.

Livembe alisisitiza kwamba wawekezaji wawili binafsi wanaoendesha bandari hiyo, wamechangia kwa kiwango kikubwa kuboresha ufanisi wake kiutendaji.

Alisema kuwa muda wa kawaida wa kutoa mizigo kutoka kwenye meli moja umepungua kwa kiasi kikubwa kutoka wastani wa siku 23-24 hadi wastani wa siku tatu pekee.

Kusimikwa kwa mitambo ya kisasa ya kubeba mizigo na mashine zinginezo kumeongeza uwezo wa bandari hiyo katika kushughulikia mizigo.

"Ufanisi katika Bandari ya Dar es Salaam umepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za usafirishaji, hivyo kutoa nafuu kwa watumiaji wa mwisho," alisema Livembe.

Kaimu Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Abeid Ngalusi, alikiri uwekezaji huo umeboresha shughuli za bandari hiyo.

Alisema kuwa muda wa meli kusubiri kuingia bandarini umepunguzwa hadi sifuri (meli inaingia bandarini moja kwa moja badala ya kusubiri), huku muda wa kupakua mizigo ukiwa umepungua kutoka wastani wa siku 10 hadi siku tatu.

Hata hivyo, Ngalusi alibainisha changamoto mpya za wasafirisha mizigo wengi hawaondoi mizigo yao kwa wakati, jambo linalosababisha msongamano.

"Bandari si kituo cha kuhifadhi mizigo," alisisitiza. "Wasafirishaji mizigo lazima wahakikishe wanatoa mizigo yao kwa wakati ili kuachia nafasi kwa mizigo mingine."

Hivi sasa, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) inahudumia asilimia 30 ya mizigo ya ndani na asilimia 60 ya mizigo ya kupitisha kwenda nchi jirani kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Zambia na Rwanda.

Elitunu Malamia, Meneja Uhusiano wa Kampuni wa DP World, alisisitiza malengo ya kampuni hiyo kwa bandari hiyo ni kuwa ifikapo mwaka 2030, bandari itakuwa na uwezo wa kushughulikia kontena 30,000 kwa siku, likiwa ni ongezeko kubwa kutoka kiwango cha sasa.

Alisema kuwa kwa sasa, bandari inashughulikia meli 16 kwa mwezi na ina mipango ya kushughulikia kontena 220,000 katika siku zijazo.

Mnamo mwaka 2023, TPA ilitia saini mkataba wa makubaliano wa miaka 30 na Kampuni ya DP World kwa ajili ya kuboresha na kusimamia shughuli za bandari hiyo.

## Mnyukano CHADEMA waishtua LHRC

**Na Halfani Chusi**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, amesema kinachoendelea katika Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ni ishara tosha kwamba demokrasia bado ina shida nchini.

Amesema tatizo hilo pia haliko kwa chama hicho pekee bali hata Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwenye baadhi ya uchaguzi wake wa ndani huwa kunaibuka mijadala inayofafania na kinachoendelea CHADEMA.

Alisema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na Nipashe, akieleza kuwa tuhuma za rushwa ndani ya CHADEMA zinaweza kuwa za kweli au zina nia ya kumchafua mtu. Ukweli wake unaweza kuthibitika mahakamani.

"Mchakato wa kidemokrasia hapa nchini una shida, si tu kwa CCM wala CHADEMA, angalau kidogo kwa Chama cha ACT-Wazalendo huwa wanajitahidi kujiepusha na kama huwa yanatokea wana namna ya kudhibiti," alisema Dk. Anna ambaye kitaaluma ni mwanasheria.

Alisema demokrasia nchini bado ni changa na hakuna mipango ya kuifanya ikomae, huku akisisitiza suluhu ya yote hayo ni Katiba mpya.

"Tungeweza kuwa na Katiba mpya ambayo inatoa mwongozo wa kidemokrasia, Tume Huru ya Taifa Uchaguzi (INEC), ingekuwa na mwongozo ambao na wengine wangefuata. Ninadhani ingekuwa suluhu kwa ukuzaji wa demokrasia nchini.

"Ukiona mzazi ana changamoto basi hata watoto lazima watakuwa nayo, pia katika uchaguzi wa CHADEMA, nimeona wanaume wengi wamechaguliwa katika nafasi mbalimbali. Hii inaonesha nafasi ya wanawake ndani ya chama hicho bado ni ndogo," alisema Dk. Anna.

Alishauri kuwe na mabadiliko makubwa ya kisheria ili kuwa na demokrasia katika uchaguzi japo ni ngumu kwa sasa kwa sababu vitu vingi vimo katika Katiba.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Msimamizi wa kituo cha upimaji wa watoto wenye ulemavu, Mwalimu Neema Mukama (kulia), akizungumza na wazazi wenye watoto wenye mahitaji maalumu kwa ajili ya kuwatambua na kuwaandikisha shule ya msingi iliyopo Nzuguni B, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Video za rushwa mtandaoni zazua balaa polisi

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limewakamata askari wawili wa usalama barabarani (trafiki) kwa tuhuma za kupokea rushwa kutoka kwa madereva wa mabasi ya abiria, maarufu kama daladala.

Jana katika mitandao ya kijamii ilisambaa video ikionyesha askari hao wakipokea kinachodaiwa kuwa ni rushwa kutoka kwa madereva na makondakta wa daladala waliowasimamisha kutokana na makosa ya kukiuka sheria za usalama barabarani.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alisema askari hao, Koplo John na WP Koplo Mgisi, wameshawaakamata na kwa sasa wako mahabusu.

Alisema hatua za kinidhamu za mashtaka ya kijeshi zimeshaanza kuchukuliwa dhidi yao wakati wakisubiria hatua zingine za kisheria.

Kamanda Muliro alisema wakati askari hao wakitekeleza majukumu yao, walifanya vitendo hivyo ambavyo ni kinyume cha maadili, hivyo kuchafua taswira ya Jeshi la Polisi na serikali.

"Askari hawa tayari wamekamatwa, wako mahabusu na hatua kali za kinidhamu za mashtaka ya kijeshi zimeanza kuchukuliwa, " alisema.

Kwa mujibu wa Muliro, jeshi hilo litaendelea kuchukua hatua kali na za haraka na halitavumilia vitendo vyovyote vya kulidhalilisha au vilivyo kinyume cha maadili ya jeshi hilo.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Watoto walioibwa wakutwa mafichoni kwa sangoma

**Na Maulid Mmbaga**

WATOTO wawili wanaodaiwa kuibwa na kutoroshwa na dada wa kazi za ndani kwa kushirikiana na mganga wa kienyeji katika eneo la Tandika Wilaya ya Temeke, mkoani Dar es Salaam siku chache zilizopita wamepatikana katika mazingira ya kutatanisha.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, kamishna Msaidizi mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alisema jana kuwa Watoto hao ni Husna Gulam mwenye umri wa miaka mitatu na Mahdi Mohamed wa miaka minne, waliibwa nyumbani kwao, Tandika na baada ya upelelezi kufanyika kwa takribani siku tatu, walipatikana nyumbani kwa mganga, Abdulkarim Shariff (43), Kimara Baruti, Ubungo mkoani Dar es Salaam.

Alisema baada ya watoto hao kupatikana, walipelekwa hospitalini kwa ajili ya kufanyiwa vipimo ambako hawakukutwa na tatizo lolote na kwamba watakabidhiwa kwa wazazi wao wakati shauri hilo uchunguzi wake ukikamilishwa ili watuhumiwa wafikishwe kwenye vyombo vya kisheria.

"Watuhumiwa hawa ambao wamekamatwa wanahojiwa kwa kina ili kujua malengo na dhamira zao zilikuwa ni nini hadi kufanya tukio hilo la wizi wa watoto. Jeshi linatoa wito na ushauri kwa watu wanaotaka kuajiri au walioajiri wasaidizi wa kazi za ndani kujua historia na tabia zao na kufahamu wametoka wapi kabla ya kuwaajiri na kuwaweka kwenye nyumba zao.

**"Kutojua historia, tabia na eneo analotoa msaidizi wa ndani na kumweka ndani ni sawa na kujiwekea hatari iliyofichika katika nyumba yako. Watuhumiwa hawa watafikishwa katika mamlaka zingine...**

"Kutojua historia, tabia na eneo analotoa msaidizi wa ndani na kumweka ndani ni sawa na kujiwekea hatari iliyofichika katika nyumba yako. Watuhumiwa hawa watafikishwa katika mamlaka zingine za kisheria haraka iwezekanavyo ili hatua za kisheria zichukuliwe," alisema Muliro.

Baba wa watoto hao, Mohamed Kassim, alisema baada ya watoto hao kuibwa, hatua ya kwanza alijirekodi kipande cha video na kukichapisha mtandaoni hatua iliyosaidia taarifa kuwafikia wengi likiwamo Jeshi la Polisi ambalo liliwasaidia kwa kiasi kikubwa hadi kufanikisha kuwapata wanawe.

"Watoto walipotea tangu Januari 11, mwaka huu, na jana (juzi) tulipokea taarifa kwamba twende Kituo cha Polisi Chang'ombe ili kuwatambua watoto wetu. Tulienda na tuliwakuta pale lakini ni namna gani walipatikana walishafafanua.

"Kuhusu dada wa kazi, mimi hata nilikuwa simjui kwa sababu alipatikana na alikaa siku nne tu ndipo tukio hilo likatokea.

Nina imani Jeshi la Polisi lina mkono mrefu litamkamata ili atueleze alikuwa na nia gani kuwachukua watoto," alisema Kassim.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA NJONBE, RUKWA, SONGWE NA RUVUMA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA ZA NYASA, MBINGA, MJI WA MBINGA, WILAYA YA SONGEA NA MANISPAA YA SONGEA.**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza na route ya tisa utafanyika katika Mikoa ya Njombe, Rukwa, songwe na Ruvuma katika Halmashauri ya Wilaya za Nyasa, Mbinga, Mji wa Mbinga, Wilaya ya Songea na Manispaa ya Songea tarehe 12 hadi 18 Januari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari litafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. SIKU: Uboreshaji utafanyika kuanzia siku ya Jumapili tarehe 12 hadi siku Jumamosi tarehe 18 Januari, 2025.
2. VITUO: Uboreshaji utafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji.
3. MUDA: Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi ambao hawakuwahi kuandikishwa hapo awali, na ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka
2. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi (Jimbo au Shehia).
3. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
4. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
5. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili kwa pamoja, wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la shehia anayokusudia kuhamia, kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo katika kituo cha kuandikisha Wapiga Kura ili kukamilisha taratibu na kupatiwa kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika katika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo (maarufu kama kitochi au kiswaswadu) anaweza kuingia kwenye mfumo wa OVRS kwa kupiga *152*00#, kisha, atachagua namba 8 na kubonyeza, kisha atachagua namba 2, kisha atabonyeza namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga simu namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali na hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa leo tarehe 03 Januari, 2024 na:

**Kailima, R. K**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Crispin Chalamila (kushoto) akizungumza na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusuph Mwenda, jijini Dar es Salaam juzi, yakilenga kuongeza ushirikiano wa kuhakikisha kodi inakusanywa kikamilifu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT yapuliza kipenga watiania udiwani, ubunge na urais 2025

**Na Mwandishi Wetu**

ACT-Wazalendo imetangaza kuanza kwa mchakato wa ndani ya chama wa wanachama kujitokeza na kutangaza nia ya kugombea nafasi mbalimbali za Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu kuanzia jana.

Hatua hiyo ni utekelezaji agizo la Halmashauri Kuu ya Chama Taifa iliyoelekeza chama kuweka utaratibu wa wanachama kutangaza nia ya kugombea nafasi za udiwani, udiwani wa viti maalumu, ubunge, ubunge wa viti maalumu na urais.

Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu alitangaza kuanza kwa mchakato huo jana alipokutana na waandishi wa vyombo vya habari kwenye ofisi za Makao Makuu ya chama mkoani Dar es Salaam.

Alitaja mambo ya kuzingatiwa kwenye mchakato huo ni pamoja na watiania kutakiwa kujisajili kwenye orodha ya watiania kwa ngazi husika kwa kujaza fomu maalumu.

"Watiania wa udiwani na udiwani wa viti maalumu watajaza fomu ngazi ya kata, ubunge na ubunge wa viti maalumu ngazi ya jimbo na watiania wa urais watajaza fomu maalumu Ofisi ya Makao Makuu ya chama," alifafanua.

Ado alisema watiania wanaruhusiwa kujitangaza kupitia njia mbalimbali ikiwamo kuzungumza na waandishi wa habari. Idara ya Habari, Uenezi na Uhusiano na Umma Ngazi ya Taifa kwa kushirikiana na viongozi wa mikoa na majimbo imeagizwa kuhakikisha kuwa watiania wote wanapata nafasi ya kujitangaza kupitia kurasa za mitandao ya kijamii ya chama na kuwaunganisha na waandishi wa habari na kusambaza taarifa za watiania hao.

Katibu Mkuu Ado alisema viongozi wa mikoa, majimbo na kata wameagizwa kuwaruhusu watiania kutumia ofisi za kata, majimbo na mikoa kutangaza nia zao. Kwa ngazi ya urais wa Tanzania, watiania wanaruhusiwa pia kutangaza nia kupitia Ofisi ya Makao Makuu ya chama.

"Watiania wanapaswa kujipima kwa kuzingatia vigezo vya watiania ambavyo vimewekwa na Halmashauri Kuu ya Chama. Vigezo hivyo ni pamoja na kutimiza sifa za kugombea nafasi husika zilizoainishwa na sheria za nchi na Katiba ya ACT Wazalendo Toleo la Mwaka 2024 pamoja na Kanuni za Uchaguzi za Chama.

"Sifa nyingine ni kuwa na haiba, maadili, uwezo wa kujieleza na maono yanayoendana na nafasi ambayo mtiania anakusudia kugombea. Watiania watapimwa pia kwa ushiriki wao katika ujenzi wa chama.

"Viongozi wa ngazi husika wameagizwa kuweka utaratibu wa kuwashirikisha watiania katika shughuli za ujenzi wa chama katika ngazi husika na kutunza taarifa za ushiriki wao," alisema.

Katibu Mkuu Ado alisema chama kitaweka utaratibu wa usaili kwa watiania kabla ya taratibu za kikatiba za uteuzi wa wagombea. Taratibu na jopo la usaili vitatangazwa baadaye kwa ngazi za ubunge na urais.

Alisema usaili huo utakuwa wazi kwa umma kupitia vyombo mbalimbali vya habari, akisisitiza kuwa wanachama wote wa ACT Wazalendo wenye sifa za kugombea udiwani, udiwani wa viti maalumu, ubunge, ubunge wa viti maalumu na urais wanakaribishwa kutangaza nia kwa utaratibu ambao umeelekezwa.

Katibu Mkuu huyo pia alisisitiza Chama cha ACT-Wazalendo kitaendeleza utamaduni wake wa kuendesha michakato ya uchaguzi kwa kuzingatia misingi ya uwazi, demokrasia na usawa.

**TUME HURU**

Alipoulizwa sababu za ACT kuamua kushiriki Uchaguzi Mkuu mwaka huu licha ya kuwapo madai ya kutokuwapo uhuru kwa wasimamizi wa uchaguzi huo, Ado alisema:

"Sisi (ACT-Wazalendo) pia hatukubaliani kabisa na tume ya sasa kwa sababu hatujaridhika na kile kilichofanyika kuifanya iwe huru. Na ndiyo maana uongozi wa chama umeshatoa kauli kuhusu hili, hata kutotambua matokeo ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopita.

"Tutapaza sauti yetu kwa kushirikiana na wadau wengine wa demokrasia kuhakikisha Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu unasimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi.

"Michakato ya ndani inaendelea kuhakikisha tunajiandaa kwa uchaguzi huo. Kama huandai wagombea, hata kama kukiwa na Tume Huru ya Uchaguzi, huwezi kufanya vizuri katika uchaguzi huo. Ndiyo maana tunajiandaa."

Kuhusu yanayoendelea katika uchaguzi wa ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na kama wako tayari kuwapokea watakaoshindwa kwenye uchaguzi huo na kuwapa nafasi ya kuwania uongozi serikalini, Ado alisema:

"Waandishi mnatumika sana, na inaonekena hili mmekubaliana hamtaliacha. Majibu yangu ni yaleyale, na leo (jana) pia ni yaleyale -- ACT Wazalendo ni chama makini cha siasa, kina mipango yake, kina mikakati yake. Ndiyo inayokifanya kuwa chama kinachokua kwa kasi zaidi nchini. Hata hao CHADEMA wanalitambua hili.

"Kitakuwa chama cha ajabu sana kikaacha mipango yake, kikaacha mambo yake na kuzungumzia yanayoendelea CHADEMA. Kwenye hili 'no comments'. Tunawatakia heri CHADEMA wafanye uchaguzi wao, wamalize salama.

"Wakitokea watu wakataka kujiunga na ACT, tunawakaribisha na tutawapokea kwa mikono miwili. Mtaji wa chama cha siasa ni watu. ACT tuko tayari kuwapokea wapiganaji wote waliokataa tamaa au wamefadhaishwa na vyama vyao.

"Ukichoshwa na CCM, CUF njoo ACT Wazalendo. Huku ndiko kimbilio la wasioridhishwa na vyama vyao. Ndiyo maana hata Maalim Seif Sharif Hamad alipoona amechoshwa na CUF, alichagua ACT.

"Kuhusu kuwapa nafasi ya kugombea, tunao wanachama wenye sifa za kugombea nafasi zote. Tunao utaratibu wa usaili wa wagombea na Mkutano Mkuu huamua nani apeperushe bendera ya chama.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Wizara yatoa kauli wanafunzi kurekodi video za utupu

**Na Jenifer Gilla**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imesema itafuatilia video ya utupu inayozunguka kwenye mitandao ya kijamii inayodaiwa kuwa ni ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Baobab iliyoko Bagamoyo mkoani Pwani ili kujua ukweli wa suala hilo.

Kauli hiyo imekuja ikiwa ni takribani wiki mbili tangu video hiyo kuzunguka katika mtandao wa kijamii wa X ikionesha wasichana hao wakiwa bila nguo na kufanya vitendo ambavyo ni kinyume cha maadili ya Kitanzania.

Video hiyo ilizua gumzo na mshangao kwa watumiaji wa mtandao huo wakihoji kuwa wasimamizi wa wanafunzi hao walikuwa wapi mpaka kufikia hatua ya kujirekodi na hatimaye kusambaa kwenye mitandao ya kijamii.

Akizungumza na wadau wa elimu Morogoro juzi, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema atatuma timu kutoka wizarani katika shule hiyo ili kufahamu imekuwaje mpaka wanafunzi hao wakafikia hatua ya kujirekodi video hiyo.

"Nitatuma na watu wangu waende pale (Baobab) inakuwaje wanafunzi wamefikia kiwango hicho," alisema.

Alisema lengo la wizara ni kuhakikisha kuwa inashughulikia masuala kama hayo ili yasijitokeze tena na si kumnyima mwanafunzi haki ya kuendelea na masomo.

"Tutazuia, tutapambana nayo, lakini hatutatuzia mwanafunzi kusoma kumnyima ufunguo wa maisha," alisema.

Kuhusu wasichana waliositisha masomo kwa changamoto mbalimbali alisema Rais alisisitiza warudi shuleni hususani waliopata ujauzito.

Hivi karibuni kumeenea tabia ya watumiaji wa mitandao ya kijamii kuweka video sizizokuwa na maadili kwenye kurasa zao kwa lengo la kuibua mijadala na kujiongezea wafuasi.

Januari 6, mwaka huu, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, Watoto na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alitoa onyo kwa waandaaji wa maudhui kuzingatia weledi na miongozo kinyume na hapo watawajibishwa kwa mujibu wa sheria.

"Kama mtu hana elimu na ufahamu kuhusu kuandaa maudhui ya mtandaoni aache mara moja maana anaharibu na atawajibishwa," alisema.

Aliwaelekeza pia wale ambao tayari wameshapakia maudhui hayo kinyume na miongozo waiondoe mara moja kabla hawajachukuliwa adhabu za kisheria.

# Wizara yatoa kauli wanafunzi kurekodi video za utupu

**Na Jenifer Gilla**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imesema itafuatilia video ya utupu inayozunguka kwenye mitandao ya kijamii inayodaiwa kuwa ni ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Baobab iliyoko Bagamoyo mkoani Pwani ili kujua ukweli wa suala hilo.

Kauli hiyo imekuja ikiwa ni takribani wiki mbili tangu video hiyo kuzunguka katika mtandao wa kijamii wa X ikionesha wasichana hao wakiwa bila nguo na kufanya vitendo ambavyo ni kinyume cha maadili ya Kitanzania.

Video hiyo ilizua gumzo na mshangao kwa watumiaji wa mtandao huo wakihoji kuwa wasimamizi wa wanafunzi hao walikuwa wapi mpaka kufikia hatua ya kujirekodi na hatimaye kusambaa kwenye mitandao ya kijamii.

Akizungumza na wadau wa elimu Morogoro juzi, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema atatuma timu kutoka wizarani katika shule hiyo ili kufahamu imekuwaje mpaka wanafunzi hao wakafikia hatua ya kujirekodi video hiyo.

" Nitatuma na watu wangu waende pale (Baobab) inakuwaje wanafunzi wamefikia kiwango hicho, " alisema.

Alisema lengo la wizara ni kuhakikisha kuwa inashughulia masuala kama hayo ili yasijitokeze tena na si kumnyima mwanafunzi haki ya kuendelea na masomo.

" Tutazuia, tutapambana nayo, lakini hatutatuzia mwanafunzi kusoma kumnyima ufunguo wa maisha" alisema.

Kuhusu wasichana waliositisha masomo kwa changamoto mbalimbali alisema Rais alisisitiza warudi shuleni hususani waliopata ujauzito.

Hivi karibuni kumeenea tabia ya watumiaji wa mitandao ya kijamii kuweka video sizizokuwa na maadili kwenye kurasa zao kwa lengo la kuibua mijadala na kujiongezea wafuasi.

Januari 6, mwaka huu, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, Watoto na makundi maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alitoa onyo kwa waandaa maudhui kuzingatia weledi na miongozo kinyume na hapo watawajibishwa kwa mujibu wa sheria.

" Kama mtu hana elimu na ufahamu kuhusu kuandaa maudhui ya mtandaoni aache mara moja maana anaharibu na atawajibishwa" alisema.

Aliwaelekeza pia wale ambao tayari wameshapakia maudhui hayo kinyume na miongozo waiondoe mara moja kabla hawajachukuliwa adhabu za kisheria.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda.

# DED apandishwa kizimbani kwa mashtaka ya uhujumu uchumi

**Na Jaliwason Jasson,** SIMANJIRO

ALIYEKUWA Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Samwel Gunzar, amefikishwa mahakamani kwa mashtaka ya uhujumu uchumi.

Warioba alifikishwa mahakamani juzi mbele ya Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Simanjiro, Charles Uisso, kujibu mashtaka yanayomkabili.

Hati ya mashtaka mahakamani hapo ilisomwa na Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), wakili Faustin Mushi.

Katika shauri hilo namba 1,048/2025, Mushi alitaja mashtaka dhidi ya Gunzar ni matumizi mabaya ya madaraka, kinyume cha kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura 329.

Alidai Gunzar anashtakiwa kwa kukiuka sheria hiyo kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022, ikisomwa pamoja na aya ya 21 jedwali la 1, kifungu cha 57 (1) na 60(2) cha Sheria ya Uhujumu Uchumi na Makosa ya Kupanga Sura 200, marejeo ya mwaka 2022.

Alidai Gunzar anashtakiwa kwa kutotimiza wajibu wa kisheria, kinyume cha Kifungu cha 123 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura 16 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Inadaiwa kuwa mshtakiwa huyo kwa nyakati tofauti alitoa zabuni ya ukusanyaji mapato ya Soko la Mnada wa Orkesume, kwa mwananchi aitwaye Elias Tipiliti, bila ya kuwapo tangazo la zabuni hiyo na bila ya zabuni hiyo kushindanishwa.

Mshtakiwa huyo alisomewa hati ya mashtaka pamoja na usikilizwaji maelezo ya awali, huku akikana mashtaka yote na yuko nje kwa dhamana.

Kesi hiyo itatajwa tena mahakamani huko Februari 11 mwaka huu kwa ajili ya kusikilizwa mashahidi wa upande wa mashtaka.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customer-relations@guardian.co.tz***




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Makandarasi wanaovurunda kazi sasa wachukuliwe hatua

**KWA** miaka mingi, makandarasi wazawa wamekuwa wakilalamika kutokupewa kazi za mradi mbalimbali ya ujenzi na badala yake wanaopewa kazi hizo ni wale wa kutoka nje.

Matokeo ya kukosa kazi hizo, kwa mujibu wa makandarasi hao ni kuendelea kuwa katika hali duni na kushindwa kuchangia pato la taifa kwa kushindwa kulipa kodi na kupata fedha za maendeleo yao.

Pamoja na kilio hicho, serikali kwa awamu tofauti, imekuwa ikiwajibu kuwa sababu kubwa kwa makandarasi hao kukosa kazi ni uwezo mdogo kwa maana ya teknolojia na kifedha kulinganisha na wale wa nje.

Pia makandarasi hao walikuwa wakikosa fursa hizo kwa kuwa mazingira yaliyokuwapo hayakutoa nafasi kwao kupata mikopo katika taasisi za fedha kwa sababu mbalimbali.

Wakati fulani, aliyewahi kuwa Rais wa Tanzania, Hayati John Magufuli, akiwa Waziri wa Ujenzi, aliwatania makandarasi hao kuwa baadhi yao hawaaminiki kwa kuwa fedha zao hazielekezwi katika miradi na kujiendeleza badala yake wanazitumia kwa anasa ikiwamo kuoa wake wengi. Pia alisema ubinafsi ni sababu nyingine inayowanyima miradi kwa sababu badala ya kuungana ili wafanye kwa viwango, kila mmoja anataka afanye peke yake ili apate fedha zote.

Kutokana na kuwapo kwa hali na mazingira hayo, serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), ilianza kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo makandarasi ili kufikia hatua ya kupewa kazi mbalimbali za ujenzi na hatimaye kupunguza kilio chao cha kunyimwa miradi. Pia baadhi ya taasisi za fedha zilianza kuwajengea uwezo makandarasi hao kwa kuwapatia mikopo ili kujiendeleza na kuwa na ukwasi utakaowapa sifa za kupata kazi.

Matokeo ya mambo hayo ni kwamba makandarasi wazawa walianza kupewa kazi za miradi ikiwamo ya ujenzi wa miundombinu ya shule, barabara, maji na usambazaji wa umeme vijijini chini ya Wakala wa Umeme Vijijini. Baadhi ya waliopewa miradi hiyo katika baadhi ya maeneo walifanya kwa ufanisi lakini wako ambao wameendelea kuvurunda na hata serikali kutishia kutowapa kazi hizo.

Mfano mzuri ni katika miradi iliyokaguliwa na kuwekwa mawe ya msingi wakati wa Mbio za Mwenge wa Uhuru ambao umekuwa ukikimbizwa kila mwaka. Katika baadhi ya maeneo miradi mbalimbali imekuwa ikikataliwa na kutokuwekewa mawe ya msingi au kuzinduliwa kwa sababu ya ama kujengwa kwa kiwango duni au kushindwa kutekelezwa kwa muda uliopangwa kwa mujibu wa mkataba pamoja na kulipwa takribani fedha zote.


Mbali na miradi hiyo, mingine ikiwamo ya maji, imekuwa ikizinduliwa kuonesha kuwa wananchi wameondokana na kero iliyokuwa ikiwakabili kwa muda mrefu lakini baada ya kitambo kidogo, maji hayatoki kana kwamba yalitegeshwa kumwonesha mgeni rasmi kwamba yapo.

Aidha, juzi kwa mfano, Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Matthew Kundo, alikataa kuweka jiwe la msingi la mradi wa maji wa Vwawa-Mlowo mkoani Songwe, unaotekelezwa na mkandarasi mzawa, kampuni ya Current Construction Ltd ya Dar es Salaam hadi kasoro mbalimbali zilizojitokeza zitakapopatiwa ufumbuzi.

Katika mradi huo ambao unatarajia kunufaisha zaidi ya wananchi 23,000 wa kata sita katika wilaya ya Mbozi, ubora wa utekelezaji wake umeibua maswali kutoka kwa naibu waziri huyo, licha ya mkandarasi kulipwa Sh. bilioni 1.3 hadi sasa.

Miradi kama hiyo iko mingi na imesababisha makandarasi wazawa ambao kwa miaka mingi walikuwa wakilia kukosa kazi, sasa wanavurunda na kuifanya serikali ifikirie vingine kwa sababu ya kutumia mabilioni ya shilingi ambayo yanapotea kwa kazi sizizo na ubora. Ufike wakati sasa watu kama hao wachukuliwe hatua stahiki zikiwamo za kisheria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tunaona madai, sarakasi za rushwa jengo la CHADEMA

Na Beatrice Moses

**NI** tuhuma za rushwa sasa zinasababisha sarakasi ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Ni kashfa wanazotupiana wenyewe.

Jambo la kushangaza zaidi linahusisha hadi viongozi wa juu, hivyo inaonyesha kugawanyika miongoni mwao, wapo wanaotuhumu wenzao kwa rushwa, pia wapo wanaohaha kusafisha waliochafuliwa.

Mcheza sarakasi aliyeiva, anaweza kuchezesha mwili hadi mifupa! Kwa kifupi, ana uwezo wa kubadili mwonekano wa umbo halisi la mwili wake, kulingana na mafunzo aliyopitia.

Ndicho kinachoonekana sasa ndani ya CHADEMA, kuna wajuzi wa kuandaa tuhuma na kuzisambaza kwa haraka hata kama ni tetesi tu hazina ushahidi, pia kuna wajuzi wa kuzikanusha.

Tuhuma zilianza kushika kasi hasa baada ya Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu, kuonyesha hofu ya kupenyezwa fedha ndani yao kutoka serikalini.

Hivyo, alilazimika kukemea suala la rushwa, akidai kuna uwezakano jambo hilo likakivunja nguvu chama kutetea haki za Watanzania.

Lissu alikaririwa akiyasema hayo Agosti mwaka huu, katika mahojiano na kipindi kimoja cha dakika 45 kilichorushwa na kituo cha televisheni nchini.

Hapo akasisitiza kwamba kuonyesha ukubwa na madhara ya tatizo hilo ndani ya chama, ndiyo maana alilazimika kulikemea.

Akabainisha kuwa na mshtuko, baada ya kuona katika wakati huu wa uchaguzi ndani ya chama hicho, kunakuwapo fedha ambazo hazijawahi kuwapo, wala kutumika katika shughuli za kawaida. Hivyo, akahisi pengine zinatoka kwenye dola kama rushwa.

Novemba mwaka jana, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, akajitokeza na kupinga madai yanayougusa uongozi wa juu wa chama.

Hoja ni kwamba, viongozi wake wa juu wamefanya makubaliano ya siri, ili chama kigawiwe madaraka kwenye muundo wa serikali au kipewe majimbo katika uchaguzi ujao.

Akasema kumeibuka tena wimbi la hoja mbalimbali ambazo zimekosa ushahidi na maeneo mengine, uchunguzi bado unaendelea, kwa kuwa CHADEMA imekuwa mstari wa mbele kupambana na ufisadi, ubadhirifu na rushwa miaka yote.

Hivyo, akatamka kwa ahadi kama chama kikiletewa ushahidi au vielelezo vya tuhuma hizo kutoka kwa mtu yeyote, watafanyia kazi haraka iwezekanavyo kwa mujibu wa katiba yao, kanuni na mwongozo wa chama dhidi ya rushwa wa mwaka 2012.

Akasisitiza kuwa mtu yeyote mwenye ushahidi au vielelezo vinavyotosheleza kuwezesha kuchukua hatua za kinidhamu kwa wahusika, awasiliane na Ofisi ya Katibu Mkuu au Ofisi ya Katibu Kanda yeyote.

Uongozi huo ukawasihi wanachama na wapenzi wao waendelee kukilinda na kukijenga chama, kirejeshe heshima yake anayodai iliporwa.

Maneno hayo pengine yalieleweka kwa baadhi yao tu, kwa kuwa bado tuhuma zilienddelea kurushwa hadi wakati huu, ambao wako kwenye mchakato wa Mkutano Mkuu wa Chama, kuna tuhuma zikiambatana na video, kudai kukamatwa kwa mgombea wa nafasi ya Katibu Mkuu wa Baraza la Vijana Chadema (BAVICHA), akidaiwa kutoa rushwa kwa wajumbe. Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika akalazimika kutoa andiko, akielezea jinsi timu ya Ofisi ya Katibu Mkuu iliyoenda kufanya malipo ya wajumbe katika Mkutano Mkuu wa BAVICHA Taifa, huku kukiwapo ufafanuzi mzito wa ziada kuhusu maofisa waandamizi kichama.

Kwa ajili ya utambuzi na uhakiki wa malipo timu hiyo, ilihusisha mwakilishi aliyeteuliwa kwa kila kanda. Kanda ya Magharibi, Katibu wake wa Kanda anatajwa kuwa mgonjwa na ofisa wake ana udhuru, hivyo walimteua mbadala, kwa jina (tunalo) awafanyie jukumu hilo.

Mnyika akaongeza angalizo lake 'kama ilikuwa sawa au la kumteua Rubibi, hilo ni suala lingine. Lakini, kwa hakika madai kuwa wajumbe wanalipwa bila tiketi wala kutia saini fomu za posho, Idara ya Fedha inayakana 'si ya kweli!"

Hapo kunatolewa sababu kwamba, fedha zilizotolewa kwa wajumbe ni zilezile za kuwarejeshea gharama zao za usafiri, pia posho za kujikimu.

Akatoa maelekezo kuwa mkutano bado unaendelea na ikiwa kuna mjumbe au mgombea ana malalamiko kuhusiana na suala hilo, ayawasilishe ukumbini kwa Msimamizi wa Mkutano wa Uchaguzi, Prof. Azaveli Lwaitama

Kwa maoni yangu, 'siasa za majitaka' hazifai, iwapo kama kuna ukweli zinatumika mahali hapo, kwa kuwa hujenga chuki miongoni mwa wanajamii, hivyo inaweza kusababisha vurugu hadi umwagaji damu.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Hal-Hikima, Nurdien Kishik, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu taasisi hiyo, kuanza maandalizi ya Mashindano ya Qur-aan, yanayotarajiwa kufanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa mwezi Machi mwaka huu. Kushoto ni Katibu Mkuu Kamati Kuu ya mashindano hayo, Salum Kiza. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kwaheri Tanzania: Kazi Tuliyoianza Pamoja Iendelee

**Na Balozi Michael A. Battle Sr.**

NINAPOONDOKA Tanzania, napenda kumshukuru kila Mtanzania kwa kunikaribisha mimi na mke wangu Linda katika nchi yenu nzuri.

Toka tulipowasili humu nchini mwezi Januari 2023, kumekuwa na matukio mengi ya kuvutia katika kipindi hiki cha miaka miwili iliyopita.

Mwanzoni kabisa mwa kipindi changu cha kuhudumu humu nchini, Makamu wa Rais wa Marekani Kamala Harris alitembelea nchini na kuwezesha kusainiwa kwa mkataba wa majadiliano ya kibiashara kati ya Marekani na Tanzania, unaounganisha sekta za umma na binafsi za Marekani na Tanzania ili kuongeza biashara na uwekezaji wa pande mbili. Ni mwezi uliopita tu, Rais Biden alisafiri kwenda Angola, ambako alikutana na Makamu wa Rais Mpango pamoja na viongozi wengine wa nchi za ukanda huu, kujadili uanzishaji wa Reli itakayokatisha Bara la Afrika (Trans - Africa Continental Railroad). Marekani ni mwekezaji mkubwa katika mradi huu, ambao utanufaisha ukanda mzima kupitia biashara iliyounganishwa zaidi.

Nikitambua kuwa uchumi imara na demokrasia imara huenda sambamba, nilijivunia sana kuwasilisha msaada wa ziada ili kuimarisha maendeleo ya mifumo ya afya, elimu, utawala wa kidemokrasia, na ukuaji wa uchumi wa Tanzania. Nilipata heshima kubwa ya kukutana na walengwa wa miradi na programu mbalimbali zinazofadhiliwa na Marekani katika safari zangu nyingi nchini kote Tanzania - mazungumzo yangu na watu wa Tanzania ni kumbukumbu nitakayoithamini sana maishani mwangu.

Mara nyingi mimi husema kwamba rasilimali kubwa zaidi ya Tanzania si dhahabu yake, wala si madini yake ya Tanzanite, au hata utajiri wake mkubwa wa wanyamapori na uzuri wake wa asili. Badala yake, rasilimali kubwa na muhimu zaidi ya Tanzania ni watu wake.

Kwa kiwango kikubwa sana,



nyakati nilizotumia kukaa na kuzungumza na vijana wa Tanzania wenye maono na hamasa, ndizo zimekuwa nyakati bora zaidi katika kipindi changu cha utumishi kama kama Balozi. Mnamo Agosti 2023, niliungana na viongozi wa vijana kutoka kote nchini walioshiriki katika Mijadala ya Demokrasia kwa Vijana. Tukio hili lililoandaliwa kwa ufadhili wa ubalozi wa Marekani lilibainisha mahitaji ya vijana wa Tanzania na kuwahimiza kushiriki zaidi katika kuimarisha demokrasia ya Tanzania.

Kwa kuwekeza katika akili na fikra changamfu za vijana wa Kitanzania na kuwapa zana na uwezo wa kufanikiwa, tunawekeza katika mustakabali wa Tanzania wenye mafanikio. Ndiyo maana tunahakikisha Watanzania wengi zaidi wanapata fursa ya elimu yenye ubora wa juu katika vyuo vikuu vya Marekani.

Ndiyo maana tulileta Shindano la Teknolojia la Marekani na Tanzania (U.S.-Tanzania Tech Challenge) nchini Tanzania, tukiwekeza katika mawazo mazuri ambayo wabunifu wa teknolojia wa Tanzania tayari wameyabuni. Zaidi ya wabunifu 100 wa teknolojia walituma mapendekezo ya kuendeleza ushiriki kamilifu wa kiraia kwa Watanzania kwa kutumia zana za kiteknolojia.

Ndiyo maana tulitetea kurejesha mradi wa awali wa Changamoto za Milenia (Millennium Challenge Corporation - MCC) nchini Tanzania, ili kusaidia mustakabali wa kidemokrasia kwa Watanzania wote.

Hiyo pia ndiyo sababu niliendelea kutoa kauli za wazi hadharani na kwa faragha kwa ajili ya kuendeleza demokrasia ya Tanzania. Hayo niliyafanya kwa sababu utawala wa kidemokrasia wa Tanzania hautaifanya Tanzania kuwa huru na yenye usawa tu, bali pia utaifanya nchi hii kuwa tajiri zaidi na yenye uwezo wa kutumia kikamilifu zaidi rasilimali yake muhimu zaidi - watu wake.

Ndiyo maana Marekani ni mshirika mkubwa zaidi wa maendeleo wa Tanzania. Na tutaendelea kuwekeza katika kuimarisha sekta ya afya, kupunguza vifo, na kuinua ubora wa maisha ya mamilioni ya Watanzania. Kupitia PEPFAR, tunaunga mkono na kuwasaidia wale wanaoishi na VVU/UKIMWI kuishi maisha yenye afya na ustawi, huku tukidhibiti maambukizi, faida ya kiafya ambayo vizazi vijavyo vya Watanzania vitaendelea kunufaika nayo.

Nimetembelea pembe zote za nchi hii na kukutana na watu wa hali na makundi ya aina mbalimbali. Nimevutiwa na kustaajabishwa sana na jinsi Watanzania wanavyojitoa kwa dhati kuishi katika misingi ya umoja, utu, na ushirikiano.

Tanzania iliyo na umoja, inayozingatia kwa dhati heshima na utu wa kila raia, ni Tanzania itakayoathiri dunia kwa njia chanya. Hiyo ilikuwa ndoto ya Mwalimu Nyerere, na ni ndoto nitakayoitunza moyoni mwangu hata baada ya kuondoka Tanzania.

Daima nitauenzi muda wangu hapa Tanzania. Na nitayaweka moyoni mwangu, katika maisha yangu yote, mafunzo mengi niliyopata kutoka kwa watu wa Tanzania.

Imekuwa heshima kubwa sana maishani mwangu kuhudumu kama Balozi wa Marekani nchini Tanzania.

# Mtendaji kijiji asimamishwa madai ya ulevi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

OFISA Mtendaji wa Kijiji cha Nganulwa wilayani Shinyanga, Sebastian Tungu, amesimamishwa kazi kwa tuhuma za kuwa mlevi wa muda wote, hivyo kushindwa kuwahudumia wananchi.

Sakata hilo lilitokea juzi kwenye mkutano wa hadhara wa Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Julius mtatiro,wakati akisikiliza kero za wananchi wa kijiji hicho na kuzitatua.

Alisema haiwezekani serikali kuendelea kuwa na mtumishi ambaye ni mlevi, hivyo kumwagiza Ofisa Utumishi wa Wilaya ya Shinyanga, kumwondoa Mtendaji huyo kutofanya kazi tena kijijini humo na kumtafutia majukumu mengi nje ya kijiji hicho.

"Hatuwezi kuendelea kuwa na mtumishi mlevi huyu tunamuondoa leo na ataletwa mwingine, na kuagiza Ofisa Utumishi, mtendaji huyu wa kijiji mpangie majukumu mengine nje ya kijiji hiki," alisema Mtatiro.

Aidha, aliwataka watumishi wa serikali kila mmoja awajibike katika eneo lake kwa kufanya kazi na siyo kusubiri msukumo wa viongozi kutoka juu, bali wafanye kazi kwa mujibu wa taratibu na miongozo ya utumishi, ikiwamo kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua.

Katika ziara hiyo mkuu wa wilaya alisikiliza kero mbalimbali za wananchi zikiwamo za ukosefu wa maji, umeme, migogoro ya ardhi na ubovu wa miundombinu ya Barabara na kuahidi kila moja litatatuliwa kwa wakati wake.

Nao baadhi ya wananchi wa kijiji hicho, awali waliiomba serikali kuwatatulia kero zao ambazo wamekuwa wakiziwasilisha mara kwa mara bila ufumbuzi.

Kadhalika walitaka serikali kumwondoa mtendaji huyo ambaye amekuwa hatatui shida zao kutokana na muda wote kuwa mlevi wa pombe.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Waziri agoma kuweka jiwe la msingi mradi wa maji

**Na Mosea Ng'wat,** MBOZI

NAIBU Waziri wa Maji, Mhandisi Kundo Mathew, amegoma kuweka jiwe la msingi la mradi wa maji wa Vwawa-Mlowo mkoani Songwe, unaotekelezwa na mkandarasi mzawa, kampuni ya Current Construction Ltd ya Dar es Salaam.

Mhandisi Kundo amegoma kuweka jiwe hilo mpaka changamoto zilizopo zitakapotatuliwa.

Mradi huo ambao unatarajia kunufaisha zaidi ya wananchi 23,000 wa kata sita katika wilaya ya Mbozi, ubora wa utekelezaji wake umeibua maswali kutoka kwa naibu waziri huyo, licha ya mkandarasi kulipwa Sh. bilioni 1.3 hadi sasa.

Mhandisi Kundo alichukua uamuzi huo juzi katika siku ya pili ya ziara yake ya siku mbili mkoani Songwe baada ya kusomewa taarifa ya maendeleo ya utekeleza kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vwawa-Mlowo (VWAMWASSA), Mhandisi Clavery Casmir.

Akikagua mradi huo, Kundo hawezi kuidhinisha hatua hiyo ya uwekaji wa jiwe la msingi hadi kero katika utekelezaji wa mradi huo zitakapopatiwa ufumbuzi.

"Niko tayari kupewa majina mabaya lakini kwa mradi huu siwezi kuweka jiwe la msingi, Mameneja (wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini- RUWASA) wa wilaya, hata mngekuwa mnatekeleza wenyewe, msingefanya kazi chafu kama hii," alisema.

> **"Niko tayari kupewa majina mabaya lakini kwa mradi huu siwezi kuweka jiwe la msingi, Mameneja (wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini- RUWASA)...**

Mradi huo unahusisha kazi mbalimbali kama uchimbaji wa kisima cha maji eneo la Hasanga, ujenzi wa matangi mawili ya maji yenye ujazo wa lita 250,000 na 75,000, ulazaji wa mabomba yenye urefu wa mita 51,600 na ununuzi wa vifaa mbalimbali kama transfoma, jenereta, na pikipiki tano kwa ajili ya usimamizi.

Mhandisi Kundo alibainisha kuwa baadhi ya kazi zimetekelezwa chini ya kiwango huku akisisitiza kuwa serikali inaamua kuwapa makandarasi wa ndani fursa ya kujenga uchumi wao lakini wanapaswa kuhakikisha kazi zao zinakidhi viwango vilivyowekwa.

"Hatuwezi kuona Rais analeta zaidi ya Sh. bilioni mbili ili kutatua changamoto za wananchi, halafu mradi unakosa ubora na kuwa changamoto, hivyo ni lazima ziondolewe kwanza ndipo nitakuja kuuzindua rasmi," aliongeza.

Kutokana na hali hiyo, Mhandisi Kundo aliiagiza Bodi ya VWAMWASSA na RUWASA kumsimamia mkandarasi huyo ili afanye marekebisho kwa kasoro zote zilizobainika na miradi mingine mkoani Songwe.

Mwenyekiti wa Bodi ya VWAMWASSA, Simon Mboya, alikubaliana na hatua iliyochukuliwa na Naibu Waziri na kuahidi kuwa suala hilo litawasilishwa kwenye vikao vya bodi kwa uamuzi zaidi.

Mradi huo ulioanza Machi, 2023 ulikuwa ukamilike Februari, mwaka huu, lakini kasoro hizo zimetia shaka juu ya kukamilika kwa wakati.

# Maliasili, Mambo ya Ndani wapewa somo kukuza utalii nchini

**Na Happiness Shayo,** DODOMA

WIZARA ya Maliasili na Utalii imetakiwa kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika kukuza soko la utalii nchini na kurahisisha utoaji wa huduma ya viza kwa watalii.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Timotheo Mnzava, alisema hayo juzi katika kikao kilichofanyika Bungeni jijini Dodoma.

"Wizara ya Mambo ya Ndani, Uhamiaji na Wizara ya Maliasili na Utalii mshirikiane kukuza sekta ya utalii. Tunahitaji mfanye zaidi kuisaidia sekta hii na kama kuna changamoto mkazitatue," alisema.

Mnzava amezitaka Wizara hizo kuoanisha mifumo ya malipo kwa watalii na kuweka mikakati madhubuti ya kutambua masoko muhimu ya watalii na kuwavuta waje nchini sambamba na kurahisisha michakato ya kupata viza kwa watalii hao.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, aliiahidi kamati hiyo kwamba wizara yake itahakikisha inafanya kazi kwa ukaribu na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhakikisha soko la utalii linakua ili kuunga mkono juhudi za serikali kukuza sekta ya utalii nchini.

"Tutahakikisha tunatambua masoko muhimu ya utalii na kuweka mikakati madhubuti ya kuvutia watalii kwa kushirikiana," alisema Balozi Chana.

Kikao hicho kilihudhuriwa na viongozi na watendaji mbalimbali kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi zake na viongozi kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Idara ya Uhamiaji.



Ofisa Tarafa ya Katerero, Bukoba mkoani Kagera, Bwanku Bwanku (kulia), akikabidhi vifaa vya shule na fedha kwa mwanafunzi Lameck Gibson anayeingia darasa la nne katika Shule ya Msingi Lyamahoro A katika kijiji cha Nyakigando, Kata ya Kaibanja juzi, baada ya kuona kwenye mitandao ya kijamii akiomba msaada wa vifaa hivyo. Katikati ni mama wa mwanafunzi huyo, Winifrida Gibson. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 628,000 wapatiwa msamaha matibabu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAGONJWA 628,417 wakiwamo watoto chini ya umri wa miaka mitano na wajawazito waliokuwa wakipatiwa matibabu katika Hospitali za wilaya mkoani Morogoro walipewa msamaha wa matibabu yenye gharama ya Sh. bilioni 4. 074 katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2024.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Prisca Gallet, alisema hayo jana wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) kilichoongozwa na Mkuu wa Mkoa, Adam Malima.

Alisema kati ya fedha hizo zilizotumika kwenye msamaha wa matibabu, Sh. bilioni 2. 212 ni za dawa pekee kwa idadi hiyo ya wagonjwa.

"Tayari tuna makundi ya msamaha wa matibabu yanaongozwa na kundi la watoto chini ya umri wa miaka mitano asilimia 45, wajawazito asilimia 16 na wazee asilimia 15," alisema.

Dk. Gallet alizitaja halmashauri na idadi ya wagonjwa waliopewa msamaha wa matibabu kwenye mabano kuwa ni Mlimba ( 80,931), Ulanga (116,673) Mvomero (59,985) na Gairo (93,927).

Halmashauri zingine ni wilaya ya Morogoro (129,068), Manispaa ya Morogoro (45,659), Kilosa (19,619), Malinyi (66,667), Ifakara (11,275) na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro wagonjwa 4,613.

Pia alisema mkoa ulipewa ajira mpya 401 kwa mwaka 2024 na walioripoti ni 334 na wasioripoti ni 67 na miongoni mwa hao watano ni madaktari na wauguzi wakiwa 29 wa daraja la II.

Akizungumza suala la waajiriwa, Malima alimwagiza KatibuTawala wa Mkoa huo, Dk Mussa Ali Mussa, kumwandikia barua Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya ili kufanya mchakato wa kupata watumishi wengine 67 kuziba nafasi hizo.

"Serikali imetupatia ajira mpya watumishi 401 na kati yao 67 hawajaripoti na hatuwezi kuziacha nafasi hizi wazi. lazima kuletewe wengine na ni wajibu wetu kuijulisha Wizara ya Afya ituelee watimishi wengine na jukumu hilo ninamkabidhi RAS (Katibu Tawala) awasiliane na Katibu Mkuu wa Wizara," alisema Malima.



# Wafanyakazi mashamba ya maua wadai mafao

**Na Godfrey Mushi,** ARUMERU

ZAIDI ya watu 500 wanadai mafao baada ya serikali kufunga maisha ya maua wilayani hapa Mkoa wa Arusha walikokuwa wakifanya kazi miaka michache iliyopita na kupoteza ajira.

Hatua hiyo imekuja baada ya kile walichodai ni jitihada zao za kudai kulipa madai yao kugonga mwamba baada ya mashamba hayo saba ya maua kufungwa mwaka 2020 kutokana na changamoto za uendeshaji, athari za janga la UVIKO-19 na mazingira magumu ya biashara na uwekezaji.

Licha ya watu hao kulilia stahiki zao baada ya kupoteza ajira na wamiliki mitaji, serikali nayo imepata hasara kubwa kwa kupoteza mabilioni ya shilingi kutokana na kukosa kodi ya maua.

Kutokana na madai hayo, baadhi yao, akiwamo Zephania Molell, aliyekuwa mfanyakazi wa Shamba la Maua la Kili Flora Limited (Nduruma Farm), kwa nyakati tofauti jana waliiangukia Wizara ya Kilimo, iwasaidie walipwe stahiki zao, kujikimu kimaisha na kukabiliana na changamoto za kiuchumi zinazowakabili kwa sasa.

**Mwenyekiti wa Wafanyakazi wa Mashamba ya Kili Flora Limited na Mount Meru Flowers, Hamza Sulemani, alisema mpaka sasa hawajapata mafanikio yoyote.**

"Maisha yetu kwa sasa ni magumu na tuko njiapanda. Tumekusanyika hapa kuiomba serikali itusaidie kulipwa mafao yetu na malimbikizo ya madeni zaidi shilingi bilioni mbili," alisema Mollel.

Wakati, Theresa Simon, aliyekuwa mfanyakazi wa Shamba la Maua la Mount Meru Flowers, alidai baadhi ya mashamba yalifungwa kutokana na sheria, utitiri wa kodi, tozo na ushuru.

Mwenyekiti wa Wafanyakazi wa Mashamba ya Kili Flora Limited na Mount Meru Flowers, Hamza Sulemani, alisema mpaka sasa hawajapata mafanikio yoyote.

Mashamba mengine yaliyofungwa ni Tengeru Flowers, Tanzania Flowers, Shamba la Arusha Blooms.

Baada ya kuibuka madai hayo, Nipashe ilimtafuta Mwenyekiti wa Halmashauri ya Meru, Jeremiah Kishili na kuthibitisha kutambua suala hilo.

Kishili, aliwataka viongozi wa wafanyakazi hao kufikia ofisini kwake kupata ufafanuzi wa malalamiko yao.

Mwaka 2022, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliagiza serikali mkoani Arusha kuanza kufufua mashamba hayo na ikiwezekana kugawanya kwa vijana ili kujiuaji kwa kilimo wakati mchakato mwingine ukiendelea.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Serengeti, mkoani Mara, Anjelina Marko (kulia), akinusa tumbaku wakati wa uzinduzi wa mnada wa zao hilo, uliofanywa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Dk. Maulid Madeni (wa pili kulia), mjini Mugumu juzi. Katikati ni Msimamizi wa Masoko ya Tumbaku kutoka Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB), Rajabu Hassan. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasakwa kwa wizi kwenye gari Arusha

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani Arusha, linawasaka watu wanaodaiwa kwa wizi ndani ya gari aina ya Toyota Alphard, lenye namba za usajili T. 340 EJR.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, jana alisema kuwa tukio hilo lilitokea Januari 12, mwaka huu katika maeneo ya Kaloleni jijini hapa.

Masejo, alisema wameanza uchunguzi na kuwasaka watu hao baada ya Goodluck Matingisa (41) kudai kuibiwa mali zake kwenye gari hilo.

Alisema tukio hilo wamelipata kupitia picha mjongeo kwenye mitandao ya kijamii, hivyo wanaendelea na uchunguzi kuhusiana na tukio hilo na kutoa taarifa zaidi baada ya kukamilika.

"Natoa wito kwa wananchi kuacha tabia ya kubeba vitu vya thamani ndani ya magari yao bila kuwa na ulinzi na kuyaacha maeneo ya maegesho," alisema Kamanda huyo.

Aliwaomba wananchi kuendelea kutoa taarifa za watuhumiwa wa uhalifu na uhalifu ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

# DC atoa siku 14 wanafunzi kuripoti sekondari

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Fakii Lulandala, ametoa siku 14 kwa wazazi na walezi kuhakikisha wanafunzi wa kidato cha kwanza wanaripoti shule walizopangiwa, lasivyo watakamatwa na kufikishwa mahakamani.

Lulandala, alitoa amri hiyo jana wakati akizungumzia mwenendo wa kuripoti shuleni wanafunzi wa kidato cha kwanza, waliochaguliwa kujiunga na masomo kwa mwaka 2025.

Alisema mwanafunzi atakayebainika hajahudhuria masomo ndani ya siku 14 baada ya shule kufunguliwa mwanzoni mwa wiki hii, hatua kali zitachukuliwa dhidi ya mzazi au mlezi wake.

Alisema wanafunzi 3,248 wakiwamo wavulana 1,598 na wasichana 16,050 walifanya mtihani wa taifa wa kuhitimu elimu ya msingi mwaka jana.

"Zaidi ya asilimia 98 ya wanafunzi waliofanya mtihani wa kuhitimu darasa la saba mwaka jana wa 2024 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwenye shule za sekondari," alisema Lulandala.

Alisema idadi hiyo ya wanafunzi hao, inatokana na jitihada kubwa zilizofanywa na serikali kwa kuboresha miundombinu na rasilimali watu katika sekta ya elimu.

"Miundombinu ya madarasa, nyumba za walimu, vifaa vya kufundishia na walimu wa kutosha imesababisha mazingira rafiki katika shule zetu hapa Simanjiro," alisisitiza.

Vilevile, alisema kata zote 18 za Simanjiro zina shule za sekondari na nyingi ziko karibu na makazi ya watu.

"Ifikapo Januari 27 kwa maana ya wiki mbili, watoto wote wafike shule, wasizuiwe kwa kukosa mahitaji ikiwamo sare kwa kuwa jukumu la vifaa vya shule ni la mzazi au mlezi," alisema Lulandala.

Mkazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Elia Baraka, ameipongeza Kamati ya Maendeleo ya Kata ya Endiamtu kupitia Diwani wake, Lucas Zacharia, walivyojitoa kusaidia kuchangia gharama za madawati ya Shule ya Sekondari Mirerani B.W. Mkapa.

"Kutokana na upungufu wa madawati kwenye shule hiyo, wazazi na walezi watachangia Shilingi 20,000 badala ya Shilingi 35,000. Tunampongeza Diwani Luka kwa kuchangia nyongeza hiyo," alisema Baraka.

Mkazi wa Kijiji cha Naberera, Sinyati Mollel, alisema serikali inapaswa kuchukua hatua kwa wazazi na walezi watakaobainika kuozesha binti zao ambao ni wanafunzi.

"Kuna baadhi ya wazazi na walezi wanapokea mifugo kama mahari na kuwaozesha mabinti zao badala ya kuwapeleka shule wakasome, serikali iwe macho kwenye hilo," alisema Sinyati.





## Viongozi wa ushirika watakiwa kuwainua wakulima kiuchumi

**Na Timothy Itembe,** TARIME

CHAMA Kikuu cha Ushirika cha Wakulima Mkoa wa Mara (WAMACU) kimewataka viongozi wa vyama vya ushirika kuelekeza nguvu zao kuwasaidia wakulima kuinuka kiuchumi.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Meneja Mkuu wa WAMACU, Samwel Gisiboye wakati akizungumza na viongozi na wakufunzi wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC) waliopo mkoani Mara kwa ziara ya mafunzo kwa vitendo na kutoa ushauri wa kutunza amani na usalama kwa manufaa ya wananchi na Taifa.

Giseboye, alisema wakulima wanahitaji kuwezeshwa katika sekta mbalimbali na kuelimishwa ili kuleta mabadiliko kwa kuendesha kilimo cha kibiashara na kukuza uchumi.

Aliupongeza uongozi wa chuo hicho kwa kuwa wa kwanza kuwatembelea na kuwataka kuona namna ya kuongeza fani ya kilimo katika chuo chao ili kupanua wigo wa ajira kwa wahitimu wao nchini

Aliwasihi katika maeneo yote wanakofanya ziara kunadi ajenda ya kilimo ili kuleta tija kwa taifa, kuongeza uzalishaji wa mazao na kuzalisha ajira.

Mkuu wa Msafara huo, Brigedia Jenerali Baganchwera Rutambuka, alikitaka chama hicho kujikita katika dhima waliyonayo ya kuwasaidia wakulima ili kuwainua kiuchumi kupitia mazao ya biashara.

Rutambuka, alikitaka chama hicho kuendelea kujikita kuwasaidia na kuwainua wakulima kwani kwa kufanya hivyo, watakuwa wamelikomboa Taifa kupitia Sekta ya Kilimo.

"Lengo letu ni kupita kuangalia amani na usalama wa jamii na mikakati ya Taifa hususani usalama wa mipaka kwa hali hiyo WAMACU jikite kwenye kilimo na si vingine," alisema.

# Vikwazo wanafunzi kidato cha kwanza vyalegezwa

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

IKIWA ni siku ya nne tangu kufunguliwa kwa shule nchini, wananchi wamejitokeza kuandikisha wanafunzi kuanza masomo ya sekondari katika shule za serikali wilayani hapa Mkoa wa Kagera bila vikwazo kwa wasiotimiza mahitaji.

Baadhi ya wazazi waliozungumza na Nipashe juu ya hali ya upokelewaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza shuleni, walisema licha ya kutokutimiza mahitaji muhimu, wanafunzi wameruhusiwa kuendelea na masomo huku wakipewa muda wa kujipanga kukamilisha.

Mkazi wa Kata ya Kashai, Malselina Simon, alisema ametimiza baadhi ya mahitaji ya shule na kumpeleka mtoto wake kuanza masomo, licha ya kupungukiwa sare muhimu na kupokelewa.

Malselina, alisema alikuwa amepanga kusitisha kumpeleke mtoto wake shule hadi atakapotimiza mahitaji yote, lakini alipokea wito wa kutakiwa kupeleka vyovyote alivyo.

Alisema huo ni msaada mkubwa kwa wazazi na walezi wasiokuwa na uwezo hasa katika kipindi hiki cha mwanzoni mwa mwaka 2025.

"Kwa sasa mwanafunzi hawezi kukataliwa kuingia darasani kuanza masomo endapo anaonekana kuwa na mapungufu ya mahitaji, tutajitahidi pale ambako hatujakamilisha wakati watoto wakiendelea na masomo," alisema. Mkazi wa Kata ya Bilele, Zainab Hamdan, alisema licha ya kuwepo kwa mapungufu kumpeleka mwanafunzi shule, kunakusikilizwa mzazi hadi atakapo kamilisha.

"Awali tulikuwa na uwezo wa kupata fedha lakini kwa sasa hali ni ngumu hivyo hatua ya kuruhusu tupeleke watoto hata bila kumaliza michango imekuwa msaada zaidi kwetu wazazi," alisema Hamdan

Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Kashai, Renard Katabazi, alisema mwitikio wa wanafunzi kuripoti kuanza kidato cha kwanza katika muhula huu wa masomo upo juu katika kipindi kifupi.

**Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Kashai, Renard Katabazi, alisema mwitikio wa wanafunzi kuripoti kuanza kidato cha kwanza katika muhula huu...**

Katabazi, alisema hadi kufikia juzi wanafunzi 141 kati ya 465 walikuwa wameripoti shuleni hapo na kuanza masomo, kati ya hao, wasichana 231 na wavulana 234.

Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Erasto Sima, alisema katika wilaya hiyo waliochaguliwa kujiunga na kidato kwanza mwaka huu baada ya kufaulu mtihani wa taifa wa darasa la saba mwaka jana ni 6,398, kati ya hao, wavulana 3050 wasichana 3348.

Sima, alisema wanafunzi waliochukua fomu kwa ajili ya kujiunga kidato cha kwanza katika shule za sekondari za serikali wilayani humo ni 4,780.



Mkulima wa Kata ya Mondo, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, Neema Maziku, akiwa ameshikilia moja ya jembe la kukokotwa na ng'ombe, yaliyotolewa na Shirika la Dorfra Co. Ltd kwa gharama ya 50,000/- badala ya 200,000/- kwa lengo la kuinua uzalishaji wa zao la mpunga na kuwainua kiuchumi wakulima wanawake, katika hafla iliyofanyika Shule ya Msingi Mbulu, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wakulima wanawake wa mpunga wajikongoja

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA wanawake wa mpunga katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga wamesema gharama kubwa za zana za kilimo ni kikwazo kwao kujiendesha kibiashara na kuzidi kudidimia kiuchumi kwa kupata hasara.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, mmoja wa wakulima hao kutoka Kata ya Mondo, Neema Maziku, alisema wanalazimika kuendesha kilimo cha kawaida kwenye eneo dogo licha ya kuwa na maeneo makubwa na kupata mavuno 'kiduchu'.

Neema, aliwaomba wadau wa kilimo kushusha gharama za pembejeo ili kukidhi mahitaji kama njia ya kuwasaidia kuachana na kilimo cha kutumia jembe la mkono kwenye mashamba makubwa.

Mary Mganga wa Kata ya Busoka alisema pamoja na serikali kuweka ruzuku kwenye pembejeo za kilimo, hawana elimu ya matumizi yake na kuwa miongoni mwa sababu za kukosa mavuno ya kutosha.

Kwa mujibu wa Mary, wakulima hao hawafahamu muda gani wanatakiwa kuweka mbolea ya kukuzia, kuondoa magugu shambani na dawa ya kuua wadudu.

Alisema kukosekana kwa elimu hiyo kwao ni janga kwa kudidimia kiuchumi kwa kuvuna magunia 15 ya mpunga kwa hekari badala ya 40 mpaka 50.

"Pia jembe la mkono sokoni linauzwa Sh.7,000 mpaka 10,000 ambao linatumika kulima eneo dogo, jembe linalokokotwa na ng'ombe linauzwa kwa Sh.200,000 gharama ambayo ni kubwa kulingana na hali zetu," alisema Mary.

Katika kuwasaidia wakulima wa hali duni wilayani hapa, Shirika lisilo la kiserikali la Dorfra Co.ltd kwa kushirikiana na Shirika la Meda wameanza kusambaza zana za kilimo kwa robo gharama na kutoa mafunzo kwa wakulima ili kupandisha thamani ya zao la mpunga na kuinua uchumi wa wakulima wanawake


Meneja wa Dorfra Co.ltd, Bakari Juma alisema kati ya Novemba 27 na 29 mwaka jana walitoa zana hizo kwa wakulima 525 wa kata 20 za Manispaa ya Kahama na kuwapatia elimu ya kilimo cha kisasa.

Alisema elimu hiyo ni namna ya kulima kisasa, kanuni bora za kilimo, mbegu bora, utayarishaji wa shamba, matumizi sahihi ya mbolea, udhibiti wa magugu kwa kutumia dawa, magonjwa sumbufu na kupanda kwa kuzingatia mstari.

Alisema wanawapatia wakulima hao majembe ya kukotwa na ng'ombe kila mmoja kwa gharama ya Sh.50,000 badala ya bei ya sokoni Sh.200,000 ili kuhakikisha wanaongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.


Mkuu wa Divisheni ya Kilimo na Uvuvi wa Manispaa hiyo, Pendo Matulanya, aliwataka wakulima hao kuwatumia maofisa ugani wa kata zao ili kupata ushauri wa namna ya kutunza shamba, kulima kisasa na muda gani wa kuweka mbolea ili kupata mavuno ya kutosha.

ama
ALHAMISI JANUARI 16, 2025
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

## Kamishna Nishati Jadidifu afunguka undani timu ya Samia ilivyojipanga



Ukurasa 12

## Barabara ya Hospitali Rufani Shinyanga inavyodhuru, inatesa wasafiri wagonjwa

# Ni mapinduzi ya utunzaji ardhi na misitu kipitia elimu kwa watumiaji

## •Kinamama wabadilishwa, washika usukani vijijini

Na Beatrice Philemon

**Alhamisi wiki iliyopita, ilikuwa na safu ya mada hii, ikiwa na dodoso la ziara yenye ushuhuda wa mwandishi katika wilaya za Kilindi, Handeni na Pangani, kuhusu mageuzi kwenye utunzaji ardhi na misitu. Fuatilia nyenzo elimu kwa jamii ilivyovusha malengo, hadi mapinduzi katika nafasi ya jinsia....**



Tukio mojawapo la upandaji miti wilayani Kilindi. **PICHA: MTANDAO**

KUNA darasa la kurejesha thamani ya ardhi na misitu mkoani Tanga linaendelea, chini ya uratibu wa kiserikali, kupitia nguzo za Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa kushirikiana na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA).

Hao wamekuja na mfumo unaowasaidia wananchi katika wilaya za Pangani, Handeni, Kilindi na Mkinga, kuvuna misitu kwa njia endelevu na rafiki wa mazingira.

Sasa wananchi wanaelimishwa matumizi bora ya ardhi na kutenga misitu ya hifadhi ya vijiji kwenye ardhi zao, ili kuboresha usimamizi endelevu wa misitu na uzalishaji endelevu wa nishati iitwayo tungamotaka, ikiwamo mkaa na mbao kwa njia endelevu.

Elida Fundi, Ofisa Utawala Bora na Uragabishi kutoka Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), anaiambia Nipashe kwamba, uvunaji endelevu ni unaokidhi mahitaji ya sasa, bila kuathiri mahitaji ya kizazi kijacho.

"Ili kukidhi mahitaji ya sasa na kizazi kijacho, serikali ya kijiji inaruhusiwa kutenga asilimia 10 mpaka 20, kwenye eneo la msitu kama eneo la uvunaji mkaa endelevu na asilimia 80 inabaki kama eneo la uhifadhi," anasema.

Pia, anaendelea: "Huyo sasa hatakiwi kufanya shughuli yoyote ya uvunaji mkaa, kilimo na shughuli nyingine, kwa ajili ya vizazi vijavyo."

**KINACHOPATIKANA**

Inatajwa hadi sasa, Suluhisho la Ujumuishaji Misitu na Nishati Endelevu ya Tungamotaka Tanzania (IFBEST), wananchi katika vijiji vya Lusane, Mnkonde, Gendagenda na Mseko ndami ya wilaya za Pangani, Kilindi na Handeni wametenga misitu ya hifadhi ya vijiji kwa uzalishaji mkaa endelevu.

Hiyo inatajwa kusaidia kuongezea kipato, kupunguza uharibifu misitu na usimamizi shirikishi, kutekeleza miradi ya maendeleo katika vijiji vyao.

Uamuzi wao wanavijiji, wametenga misitu ya hifadhi ya vijiji, baada ya kupata mafunzo ya uvunaji endelevu wa mazao ya misitu na uzalishaji mkaa endelevu, matumizi bora ya ardhi na usimamizi shirikishi wa misitu kutoka MJUMITA na TFCG.

Mafunzo yametolewa kwa wajumbe wa kamati za maliasili, viongozi wa vijiji, wafugaji nyuki, wenye misitu binafsi na wanaotaka kutetea misitu, pia wazalishaji mkaa endelevu.

Elida Fundi, ni Ofisa Utawala Bora na Uragabishi wa MJUMITA Ni mradi wa miaka mitatu unaofadhiliwa na fedha za kigeni, kupitia Wizara ya Fedha na hadi sasa unatekelezwa katika vijiji kadhaa.

Anaviorodhesha kuwa; Lusane, Mnkonde, Mswaki, Nghobore, Mkalamo, Gendagenda, Mmbogo, Mapanga na Mseko katika wilaya za Pangani, Kilindi na Handeni.

Lengo la mradi ni kuimarisha usimamizi endelevu wa mazingira kwa kuboresha usimamizi endelevu wa misitu na uzalishaji endelevu wa nishati ya tungamotaka.

**KWANINI MAFUNZO?**

Waratibu mafunzo, MJUMITA kwa kushirikiana na TFCG, wanafafanua sababu mahsusi wa mafunzo hayo ya umma, yanaangukia kuwezesha wenyeji kujua haki zao, kusimamia na kujitetea wanufaike na rasilimali zao za misitu na mazao yake.

Eneo lingine, analitaja ni zao la mafunzo liwakweze kwa uelewa na utendaji, wakazi hao kugombea nafasi mbalimbali za kiuongozi na kutendaji.

Hapo inaorodheshwa mifano ya nafasi, kama vile kamati za maliasili, uongozi wa vijiji na masuala ya misitu, ukiwa na ajenda ya kijinsia kuacha dhana 'misitu ni kazi ya wanaume' na kuleta tofauti.

Nipashe ikiwa katika ukaguzi wa kihabari eneo hili, ikashuhudia matokeo; wanawake wanashika nafasi kubwa kiungozi katika vijiji vyao kama vile Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji cha Mnkonde, wilayani Kilindi.

Vilevile, MJUMITA imezijengea uwezo asasi nyingine za kiraia za mkoani Tanga, kuweza kushawishi kuwapo mazingira wezeshi kisera, usimamizi misitu na uvunaji endelevu wa

Inaendelea Uk. 14

AFYA

# Barabara ya Hospitali Rufani Shinyanga inavyodhuru, inatesa wasafiri wagonjwa

## •Miaka mitatu ya hospitali, rekodi zinasikitisha
## •Mganga Mfawidhi, mkoa afunguka ya uvunguni...

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA




Majengo ya Hospitali ya Rufani Shinyanga. **PICHA: MTANDAO**

ILIKUWA Mei mwaka jana, mapacha Kulwa na Dotto Mahenga, wakazi wa kijiji cha Lyandu katika Manispaa ya Shinyanga, wakiwa kwenye pikipiki, walipata ajali kwa kugongwa na gari na kufariki dunia papo hapo.

Vifo hivyo vilitokea kwenye barabara iendayo Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, ambayo imekuwa ikilalamikiwa kutokana na ubovu wake, tangu kuanza kutolewa huduma katika hospitali hiyo mwaka 2022.

Mzazi wa watoto hao, Zainab Tagala, anasema kifo cha watoto wake ni pigo kubwa kwake na familia, kwani pia alikuwa akiwategemea kuendesha maisha yake, baada ya baba yao kufariki dunia, huku kaka yao mkubwa anajitegemea na familia yake.

Mama Zainab, anaeleza: "Barabara ya hospitali isingekuwa mbovu, watoto wangu sasa hivi wangekuwa wazima, yaani nikifikiria naanza kulia."

Anaendelea kwa majonzi: "Na siwezi kuzungumza tena!... Nenda ukaongee na kaka yao kwenye mji wake upo jirani tu na hapa, nasikia uchungu sana."

Nipashe inapolazimika kubadili mwelekeo, hadi kwa kaka wa vijana hao, Mohamed Shabani, anasimulia walipokea taarifa ya ajali ya wadogo zake, Kulwa na Dotto kwa mshtuko mkubwa.

Anasimulia, kwamba waligongwa wakati gari lilipokuwa ikikwepa mashimo katika barabara hiyo ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga.

Shabani anasema, aliwaacha wadogo zake nyumbani kama nguzo ya familia na baada ya vifo hivyo "wamelia na wamenyamaza" na kuomba serikali iiangalie barabara hiyo kwa jicho la tatu.

Maoni yake ni kwamba, mahali hapo panapitiwa na watu wengi na imekuwa ikikatwa na maji pale mvua zinaponyesha.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Luzila John, kila siku moja huwa wanahudumia wagonjwa zaidi ya 200.

Mwongozo wa ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga wa Mwaka 2014, unaonyesha michoro ya majengo, ikiendana na kuwapo na ubora wa barabara.

Dk. Luzila anasema, hospitali hiyo ilianza rasmi kutoa huduma za matibabu mnamo Desemba 29, 2022, hivyo hadi sasa ina miezi 24 au miaka miwili na wiki mbili.

Anasema, kutokana na uhitaji wa huduma za kibingwa kwa wananchi wa mkoa huo, ilibidi waanze kutoa huduma hivyo, licha ya ubovu huo wa barabara ulipo.

Dk. Ruzila anasema kwamba, ubovu wa barabara hiyo kutojengwa kwa muda mrefu, binafsi amekuwa akiwasilisha malalamiko yake mara nyingi, kwenye vikao mbalimbali vya viongozi.

Anataja baadhi yake ni pamoja na Kamati ya Ushauri cha Mkoa huo (RCC), akirejea kikao cha Desemba 15 mwaka 2023, lakini hakuna utekelezaji wake.

Kwa mujibu wa Dk. Ruzila, ubovu huo wa barabara, umekuwa ukisababisha vifo na kuhatarisha maisha ya wagonjwa, na kwamba magari ya wagonjwa.

"Ambulance (magari ya wagonjwa) zimekuwa zikipata ajali, huku zikiwa zimebeba wagonjwa, jambo ambalo ni hatari...

"Athari za ubovu wa barabara hii ni kubwa! Mfano ukiwa umembeba mgonjwa aliyevunjika mifupa au mjamzito, hadi kufika hospitalini hapa, atakuwa amepata maumivu makali sana na kuhatarisha afya yake," anaeleza.

Kwa mujibu wa Dk. Luzila, pia magari ya hospitali hiyo yamekuwa yakiharibika na kuingia gharama za matengenezo ya mara kwa mara na kwamba gari moja hadi sasa wamelipaki baada ya kukosa fedha za kulitengeneza.

### GARI LA WAGONJWA

Dereva wa gari la kubeba wagonjwa (ambulance) katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, John Mabelele, anataja changamoto wanazopata kutokana na ubovu wa barabara ya hospitali hiyo.

Anataja baadhi ya athari ni kuuharibika magari yao, ajali na kwamba wakuwa wakiwabeba wagonjwa wenye hali mbaya, wanailalamika kuumia.

Anafafanua kuwa, pia mvua zinaponyesha, barabara hizo zinakuwa mbaya zaidi, kwa sababu mashimo yake yanafukiwa na maji, hivyo inakuwa ngumu kwao madereva kuyaona na wanajikuta wakivunja 'shock up' za magari, huku wakiwaumiza wagonjwa.

### WATUMIA BARABARA

Safari ya kupata ufafanuzi za Nipashe, ziliifkisha kwa mgonjwa Letecia Dotto, anayeeleza uzoefu wake, akisema wanaposafiri kwa bajaji kupata matibabu hospitalini hapo, akiwa amebebwa kwenye bajaji, alikuwa akisikia maumivu makali, hasa kunapotokea mtikisiko.

Anaungana na mtumiaji barabara, Kuluthumu Mohamed, anayesema magari yao yamekuwa yakiharibika kila mara na haipiti wiki, lazima waende kufanya matengenezo, yakiwagharimu kiasi kikubwa cha fedha.

### KAULI YA RPC

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga Janeth Magomi, anaungana na kauli zilizotangulia za adha ya Barabara hiyo kuwa vyanzo vya ajali nyingi katika Manispaa Shinyanga.

"Siwezi kuchambua kwamba katika barabara hiyo zimetokea ajali ngapi, matukio haya tunajumlisha kwa ujumla," anasema TPC Magomi.

Mratibu wa ujenzi wa miundombinu ya Afya Mkoa wa Shinyanga, Faustine Mlyutu, anasema maeneo yote ya kutoa huduma za afya na kisera yanapaswa yawe na miundombinu rafiki ya wagonjwa kufika kwa urahisi penye matibabu, pasipo vikwazo.

"Kitu ambacho huwa tunakizingatia kwenye ujenzi wa huduma za afya, ni kuhakikisha miundombinu ya usafiri inakuwa rafiki kwa wagonjwa na kunapotokea changamoto huwa tunawasiliana na TARURA kufanya matengenezo ya barabara," anasema Mlyutu.



Mwonekano wa ubovu wa barabara ya kwenda Hospitali ya Rufani Mkoa wa Shinyanga, mashimo yake yameweka historia ya ajali zenye vifo. **PICHA: MARCO MADUHU**

### TARURA & MABOSI MKOANI

Meneja Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) wilayani Shinyanga, Mhandisi Samson Pamphili, anasema walishapokea maombi ya ujenzi wa barabara hiyo kutoka kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa.

Anataja tatizo linalokwamisha ujenzi wa barabara ni ufinyu wa bajeti, ila kwa sasa wamepata fedha kutoka ufadhili wa Benki ya Dunia shilingi bilioni tisa za kujenga barabara mbili, daraja na miundombinu itakayosaidia kufika hospitalini kirahisi.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, anakiri ubovu wa barabara hiyo ni tatizo kubwa kwa wagonjwa kufika kupata huduma katika hospitali ya mkoa huo.

Anasema, kwa sasa barabara hiyo imeingizwa kwenye mpango wa Benki ya Dunia na ujenzi wake unatarajiwa kuanza mwezi Februari au Machi mwaka huu.

"Barabara hii ya kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga ni mbovu sana na wananchi wamekuwa wakiipigia kelele na kipindi cha kiangazi huwa kuna vumbi," anasema Macha.

Anahitimisha kwamba "inapofika Msimu wa Masika, utelezi ni mkubwa na ina mashimo, lakini serikali ipo katika hatua nzuri ya kuijenga."

Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi ambaye pia ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Kazi, Ajira na Watu wenye ulemavu, anasema barabara hiyo ilikwama kujengwa sababu ya mifumo ya kifedha.

Anaungana kwamba, kwa sasa wanasubiri pesa kutoka Benki ya Dunia, ili waanze kutekekeza mradui wa Barabara inayofika hospitalini.

### MWONGOZO KITAIFA

Hayo yanayotokea, huku Sera ya Afya ya Mwaka 2007, kifungu cha 5 (b) kinazungumzia "huduma bora za afya zinazowafikia wananchi wote kwa urahisi," ambayo kipekee inabeba msisitizo wa kuwapo barabara bora, 'pafikike kirahisi.'

Vilevile, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, Juni 13 mwaka huu bungeni Jijini Dodoma, katika hotuba yake ya bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025, akataja takwimu; watu 7,639 wamepoteza maisha kwa ajali za barabarani kwa miaka mitano; 2019-2024, pia majeruhi 12,663.

MAZINGIRA

MKUTANO NISHATI KIMATAIFA NCHINI...

# Kamishna Nishati Jadidifu afunguka undani timu ya Samia ilivyojipanga

## •Aorodhesha mbinu, picha mavuno 'Kazi Iendelee'

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA wiki moja na nusu ijayo, Tanzania inatarajia kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu nishati, ikikusanya viongozi wa nchi 54 wa Bara Afrika.

Pia, wamo Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Umoja wa Afrika (AU), hali kadhalika mawaziri wa fedha, wanaohusika na nishati.

Katika tukio hilo litakalofanyika kuanzia tarehe 27 hadi 28, mwezi huu katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), washiriki wengine ni mabalozi, wakuu wa taasisi za kifedha za kimataifa, mazingira, nishati na sekta binafsi.

Hapo mwenyeji nchini kutaaluma serikalini, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu nchini, Innocent Luoga, ana ufafanuzi wake katika jambo hilo: "Tunamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye ameendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Nishati, juhudi ambazo zimeonekana kwa nchi na taasisi mbalimbali za kimataifa.

"Mfano hai ni kufanyika kwa mkutano huu (M300) mkubwa unaowakutanisha wakuu wa nchi zote za Afrika na wengine kutoka mataifa ya Ulaya.

"Hili ni suala la kujivunia kwa Tanzania na tunapaswa kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu kwa maono haya makubwa."

**SABABU ZA MKUTANO**

Katika ufafanuzi wake kwa wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki iliyopita, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu Innocent Luoga, anasema:

"Takwimu zinaonyesha kuwa takribani Waafrika milioni 685 hawajafikiwa na huduma ya umeme hadi sasa kati ya Waafrika zaidi ya bilioni moja.

"Kutokana na hilo Benki ya Dunia kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo Afrika wamekuja na mpango mahsusi ujulikanao kama 'Mission 300' (au M300) ambao umelenga kuharakisha upatikanaji wa umeme kwa Waafrika milioni 300 ifikapo 2030.

"Mpango huu unahusisha nchi zote za Afrika, nchi 14 zimechaguliwa kuanza utekelezaji wa mpango huu na nchi nyingine zitafuata. Kiwango kidogo cha upatikanaji wa umeme kilikuwa ni kigezo kilichotumika.

"Nchi hizo ni Tanzania, Mali, DRC (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo), Ivory Coast, Bukina Faso, Chad, Liberia, Madagascar, Malawi, Mauritania, Mozambique, Niger, Nigeria na Zambia.

"Tanzania kwa upande wake itasaini mpango huo kwa kuwa ni nchi mwenyeji wa mkutano kwani imeshapiga hatua kubwa katika usambazaji wa umeme kwa wananchi," anasema Luoga.



Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Innocent Luoga

**NAFASI YA TANZANIA**

Kamishna Luoga anaelekeza pongezi kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuipa kipaumbele sekta ya nishati, juhudi zikionekana kitaifa na kimataifa.

Hapo anarejea mfano wa kukubalika kwa taifa kufanyika mkutano ujao unaowakutanisha wakuu wa nchi za Afrika na viongozi wa nje ya bara hilo.

Hata juzi katika mkutano wake wa kufungua mwaka na mabalozi wa kigeni waliko nchini Jumanne wiki hii, Rais Dk. Samia akarudia tena hilo kuwa ni sehemu ya mafanikio yanayoshuhudiwa kitaifa, ikiangazwa katika eneo hilo la nishati.

Hadi sasa kitaifa, mbali na nishati za asili katika vyanzo vya maji kama vile Kidatu, kuna mradi mkubwa Bwawa la Mwalimu Nyerere linalotarajiwa kumaliza shida ya umeme nchini, hata kuuza kimataifa.

Maeneo mengine yanayojumuisha kupata na kutumia nishati ya gesi nchini, kazi inayoendelea, huku huduma za usambaji nisahati umeme ukifanikiwa kwa kiwango kikubwa, chini ya wakala wake maalum iliyoundwa (REA).

Wakati inapokea pesa za mradi kutoka Benki ya Dunia mnamo Novemba 2023, REA iliahidi itaiwezesha kuifikia dhamira yake ya kuvipata vijiji 12,318 vilivyolenga kitaifa ifikapo Juni 2024.

Hiyo ni kwa mujibu wa kauli ya REA wakati huo, mafanikio yakiwa mbele ya dhamira ya kipindi kilicholengwa, 2025, kwamba asilimia 70 ya Watanzania walio vijijini wafikiwe na huduma ya umeme.

Kuhusu namna taifa limejipanga kunufaika na mkutano huo wa nishati unaotarajia kuanza, Kamishna Luoga anataja orodha ya mikakati kama ifuatavyo;

Mosi, ni kuvishirikisha vyombo vya habari katika utoaji taarifa na uelewa kuhusu Mpango wa 'Mission 300' unatarajiwa kuanza.

Pili, anataja suala la kuunda timu ya wataalamu wakataondaa Mpango Mahususi wa Kitaifa uitwao 'National Energy Compact.'

Tatu, inatajwa suala la kuzishirikisha tasisisi za umma na binafsi (nafasi ya PPP), pamoja na wadau wa nishati kuhusu mpango huo, ili kupata maoni.

Nne inatajwa, ni nafasi ya kuainisha na kuandaa miradi itakayowezesha utekelezaji hup wa 'Mission 300' nchini.

Tano, Kamishna na anataja ni suala la kuandaa safu ya wataalamu watakaosimamia utekelezaji wa mpango huo; na mwisho ni namna ya kushirikiana na taasisi za kifedha katika kufuatilia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji.

**WITO WAKE**

Kamishna Luoga ana wito kuhusu ustawi wa mkutano huo, akiugawa katika maeneo kadhaa, kuanzia na wanahabari akiwasihi fursa yao kitaaluma kuelimisha kuhusu mkutano huo wa nishati, siku 11 zijazo.

"Napenda kuchukua nafasi hii kuwaomba wanahabari wote kuwa kioo cha nchi, kwa kuutangaza sana mkutano huu na kutoa habari sahihi na kwa wakati," anatamka.

Pia, anawarejea wananchi wote, akiomba ukarimu wao kwa wageni, kama ilivyo desturi ya Kitanzania, ndani ya kipindi chote cha mkutano huo ujao wa M300.



Sehemu ya mradi wa umeme wenye kiwango cha kimataifa, Bwawa la Mwalimu Nyerere. **PICHA ZOTE: MTAKTABA**

# Ni mapinduzi ya utunzaji ardhi na misitu kipitia elimu kwa watumiaji

**INATOKA UK. 11**



Wanakijiji wa Mkwaja, wilayani Pangani, katika harakati za kulinda misitu. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

nishati tungamotaka.

Pia, wanamtandao wa MJUMITA wamejengewa uwezo wa kufanya ushawishi na kutetea usimamizi shirikishi wa misitu na uvunaji endelevu wa nishati tungamotaka kutoka kwenye misitu ya vijiji iliyohifadhiwa kisheria.

Manufaa mengine, ofisa Elida anayataja ni kuwapo uzalishaji endelevu wa nishati za kuni, mkaa, wakitumiwa wanasiasa na viongozi serikali, kutatua changamoto zinazowakabili katika utekelezaji wa usimamizi shirikishi wa misitu kwenye ardhi ya vijiji.

"Tumeamua kutoa mafunzo haya baada ya kugundua kuwa misitu mingi katika mkoa wa Tanga inazidi kutoweka, watu wanazidi kuvuna miti hii kiholela kwa uchomaji mkaa, mbao, shughuli za kilimo, uchimbaji madini, ujenzi wa makazi na shughuli nyingine za kibinadamu," anasema.

MJUMITA kwa kushirikiana na TFCG zinataja kusaidia kuanzisha 'mpango wa matumizi bora ya ardhi' katika vijiji vya; Lusane, Mapanga na Gendagenda, hata kutatua migogoro kati ya vijiji iliyodumu kwa muda mrefu.

### OFISA MISITU KILINDI

Peter Mtoro, ni Ofisa Usimamizi Shirikishi wa Misitu kutoka TFCG wilayani Kilindi, anasema kupitia mradi, wananchi wamefanikiwa kutenga hekta 13,537.9 za misitu.

Hizo zinajumuisha, misitu ya hifadhi ya vijiji kwa ajili ya usimamizi shirikishi wa misitu na kusaidia wananchi kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika vijiji vyao.

Anasema, kati ya hekta hizo, jumla ya hekta 2, 304 za misitu zimetengwa kwa ajili ya uzalishaji mkaa endelevu katika wilaya ya Kilindi, Handeni na Pangani.

"Jumla ya hekta 279.1 za misitu zimetengwa katika kijiji cha Mapanga, hekta 270 zimetengwa katika kijiji cha Lusane, hekta 695 zimetengwa katika kijiji cha Mseko, hekta 800 zimetengwa katika kijiji cha Gendagenda, hekta 260 zimetengwa katika kijiji cha Mkalamo," anasema.

Anasema Wilaya ya Kilindi itazalisha tani 185.9 za mkaa endelevu kwa mwaka, wilaya ya Pangani tani 133.2 na wilayani Handeni itazalisha tani 233.3 za mkaa endelevu kwa mwaka.

Pia katika kijiji cha Mseko TFCG imewawezesha wananchi kuelewa Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu na sheria ndogo zake. Pia, wamewasaidia kuandaa mpango wa uvunaji.

"Tunashukuru Umoja wa Ulaya (European Union) kutoa fedha ambazo zimesaidia Shirika la TFCG na MJUMITA kusaidia vijiji kufanya matumizi bora ya ardhi, kutenga misitu ya hifadhi ya vijiji, kutenga maeneo kwa ajili ya makazi, mifugo, kilimo, huduma za kijamii, vyanzo vya maji na huduma nyingine, anasema.

### UVUNAJI MKAA ENDELEVU

Anasema tathmini iliyofanywa na TFCG katika msitu wa hifadhi ya kijiji cha Mseko, jumla ya vitalu 2,780 vimetengwa katika msitu wa hifadhi ya kijiji kwa ajili ya uvunaji mkaa endelevu.

Vitalu vitakuwa na uwezo wa kuzalisha magunia 2664 kwa mwaka na mapato yenye thamani ya shilingi 33,302,083 ikiwamo pia hewa ukaa.

Mbali na hilo, TFCG iliwezesha kijiji cha Mseko kufanya tathmini kujua misitu iliyopo katika kijiji chao inauwezo wa kuzalisha tani ngapi za mkaa endelevu.

Pia jumla ya wataalamu 32 kutoka halmashauri za wilaya na Tanzania Forest Services (TFS) walipewa mafunzo ili kusaidia jamii kuanzisha usimamizi shirikishi wa misitu.

### OFISA UFUATILIAJI

Ewald Emil, ni Ofisa Ufuatiliaji, Utafiti na Mawasiliano wa Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), anasema watekelezaji mradi katika vijiji husika, wameshauri kuwa vibali vyote vitakavyotolewa na halmashauri au serikali ya kijiji kwa ajili ya uvunaji endelevu wa mkaa, vitaje wavunaji weaankonda.

Anasema ni mapendekezo, baada ya kugundua vibali vinavyotolewa kusafisha mashamba, vimekuwa vikitumika kinyume na sheria.

Emil anasema, baadhi ya watu wamekuwa wakitimia vibali hivyo kuingia kwenye maeneo ya hifadhi ya misitu ya vijiji na kuchoma mkaa holela na kuchangia uharibifu misitu, huku kijiji kikikosa mapato yake.

Wameshauri utoaji wa elimu kwa makundi mbalimbali ya watumiaji wa misitu na wananchi wapatiwe shughuli mbadala ili waache kutegemea zaidi misitu kwa ajili ya kujiongezea kipato.

Pia, elimu ya uhifadhi misitu imeshauriwa iendelee kwa jamii zinazozunguka misitu, kuongeza elimu ya mpango hisa kwa vikundi mbalimbali, ikiendana na usafiri, vitendea kazi kwa kamati ya maliasili na wilaya hasa maofisa misitu na mazingira.

Pia, kuna kufanya doria kwa watu wanaoingia kwenye hifadhi ya misitu kinyume na sheria kwa ajili ya uchomaji mkaa na kilimo.

Limo, pendekezo la wananchi wanaozunguka mradi wapewe miti wapande, TFCG na MJUMITA waendelee kutoa mafunzo kwa wamiliki wa mashamba makubwa ya misitu.

Pia, viongozi wapya katika maeneo ya mradi wantakuiwa wajengewe uwezo kuhusu mradi na uhifadhi wa misitu ya asili, kama ilivyo kwa wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri.

Hiyo inatajwa kusaidia kushughulikia migogoro iliyopo kati ya vijiji, wilaya na a na kushirikisha wadau wote katika utatatuzi wa migogoro hiyo.

Mbali na hilo, uhamishaji wa mifugo, taratibu na sheria zote zizingatiwe, pia uvunaji endelevu ufanyike kwa watu wanaomiliki mashamba makubwa ya miti ili nao waweze kunufaika na mradi wa carbon.

### KUTOKA KIJIJINI

Mlezi wa MJUMITA, katika Kijiji cha Mkonde, Mwanaidi Gwalu, anaeleza: "Kupitia uhifadhi, wananchi wamejenga kisima cha maji kwa ajili ya wananchi kupitia uhifadhi wa misitu, wamepata mafunzo jinsi ya kuanzisha 'Village Community Banks' (VICOBA).

"Kutokana na mafunzo hayo, wameanzisha vikundi viwili vya VICOBA, kikundi cha Upendo na Chekanao na wameanzisha miradi ya aina mbalimbali ili kupunguza ukataji wa misitu."

Anafafanua, kabla ya kupata mafunzo, mwanzoni walikuwa wanafanya uchomaji holela wa mkaa katika msitu na kuleta madhara katika afya zao.

"Sasa hivi hawaendi kukata kuni na kuchoma mkaa ndani ya msitu, sasa hivi wanachukua mikopo kwenye VICOBA na wanafanya biashara zao," anasema

### MNUFAIKA MAFUNZO

Lucia Msongela, Katibu wa Kikundi cha Chekanao ni mufaika wa mafunzo yaliyotolewa na Shirika la MJUMITA na TFCG kupitia mradi wa IFBEST.

'Kupitia elimu niliyoipata, nimefanikiwa kukopa shilingi 500,000 kwenye kikoba na kulipa ada, hivi sasa mtoto wangu anasoma," anasema.

Hadi sasa kikundi chao kina hisa yenye thamani ya shilingi milioni tatu, yeye anafanya biashara ya kuuza na kukopesha kukopesha vitenge.


Mwanakijiji Lucia anasema, wanawake wengi hivi sasa katika kijiji chao hawaendi tena kukata miti msituni.

"Kabla ya VICOBA, hali ilikuwa ngumu, watu walienda porini kukata miti kwa ajili ya kuchoma mkaa na kuharibu msitu, sasa hivi hali ni nzuri, VICOBA vimetusaidia..." anasema.

Kuna baadhi ya wanawake wanauza bidha kama nyanya, ndizi, mboga, badala ya kutegemea kuuza kuni na mkaa.

Pia, kupitia mafunzo hayo, anataja kuwa wamefanikiwa kuanzisha mfuko wa jamii ambao hivi sasa una kiasi cha shilingi 700,000- na kuna wanachama 30, kati yao, wanaume ni wawili.

Lucia anahitimisha, kwamba kwenye biashara ya kuuza vitenge, alianza na mtaji wa shilingi 300,000 na sasa uko shilingi milioni 1.5.





# Wakulima kupewa miche milioni 20 ya kahawa

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imeanza kusambaza miche milioni 20 ya kahawa na kugawa bure kwa wakulima wa mikoa inayostawisha zao hilo ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo nchini

Mpango huo umetangazwa na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu maandalizi ya mkutano wa tatu wa nchi zinazozalisha kahawa Afrika (G25) utakaofanyika nchini mwezi ujao jijini Dar es Salaam.

Bashe, alisema miche hiyo itazalishwa katika vitu vya kahawa vilivyopo nchini na kugawa kwa wakulima ili kufikia lengo la serikali kulifanya kuwa ni miongoni mazao ya kimkakati yanayolimwa nchini.

"Serikali imeanza kusambaza miche milioni 20 kwa wakulima wadogo wa zao hilo katika maeneo mbalimbali na hii ni kuhakikisha wakulima wote wanapiga hatua kupitia kilimo hicho," alisema Bashe. Alisema kahawa ni moja ya kilimo ambacho kinaweza kuwasaidia vijana kujiajiri kupitia biashara ya kinywaji hicho katika maeneo tofauti.

**"Serikali imeanza kusambaza miche milioni 20 kwa wakulima wadogo wa zao hilo katika maeneo mbalimbali na hii ni kuhakikisha wakulima wote wanapiga hatua...**

Akizungumzia kuhusu maandalizi ya mkutano huo wa siku mbili utakaofunguliwa na Rais Samia Suluhu Hassan na kaulimbiu yake ni "Kufungua Fursa za Ajira kwa Vijana Kupitia Uboreshaji wa Sekta ya Kahawa Afrika.

Bashe, alisema mkutano huo ni matokeo ya azimio lililopitishwa katika Mkutano wa 61 uliofanyika Novemba 18 mwaka 2021 Kigali nchini Rwanda.

Alifafanua kuwa lengo ni kufanya tathmini ya mapungufu na changamoto zinazosababisha kuzorota kwa Sekta ya Kahawa Afrika. Baada ya kupitishwa kwa azimio hilo, mkutano wa kwanza wa nchi hizo ulifanyika Kenya Mei mwaka 2022 na kupitisha Tamko la Nairobi.

Tamko hilo liliweka mkakati wa kuingiza kahawa kama bidhaa muhimu ya kimkakati katika Umoja wa Afrika (AU) na agenda mwaka 2063 ya AU.

Mkutano wa pili ulifanyika Kampala nchini Uganda, Agosti mwaka 2023 na kupitisha Tamko la Kampala kuwaomba wakuu wa nchi hizo kuunga mkono kuidhinishwa na kujumuishwa kahawa bidhaa muhimu ya mkakati katika ajenda hiyo ya mwaka 2063 ya AU.



Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Singida, Martha Gwau, akizungumza katika kikao cha 48 cha Bodi ya Barabara ya Mkoa, kilichowashirikisha wabunge, wakuu wa wilaya na watendaji kutoka taasisi mbalimbali za serikali, mjini Singida jana. Mkoa huo, umetengewa Sh. bilioni 48.2 kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025, kwa ajili ya matengenezo ya barabara. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Bilioni 48.2/- kukarabati barabara Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKOA wa Singida umetengewa Sh. bilioni 48.2 kwa ajili ya ukarabati wa barabara kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025.

Mkuu wa Mkoa huo, Halima Dendego, alisema hayo jana wakati kikao cha 48 cha Bodi ya Barabara ya Mkoa kilichowashirikisha wabunge, wakuu wa wilaya, watendaji kutoka taasisi mbalimbali za serikali.

Dendego, alisema kati ya fedha hizo Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) imeidhinishiwa Sh. bilioni 29.1 na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Sh. bilioni 19.1.

Alisema katika kipindi cha zaidi ya miaka mitatu kazi zilizofanyika katika Mkoa wa Singida ni kuongeza kilometa za barabara za lami kutoka 499.28 hadi kufikia 543.09, ikiwa ni ongezeko la asilimia 43.81.

Nyingine kuongeza kilometa za barabara za changarawe kilomita 1,870.81 mwaka 2021 hadi 3,118.59 mwaka 2024/2025 na kukamilisha ujenzi wa madaraja makubwa 27, madogo 1,638, kalvati 2,341 na vivuko 65.

Dendego, aliwaelekeza wanaosimamia usafi hususani katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida kudhibiti watu kutupa takataka kwenye mitaro na kusababisha mji kukithiri kwa uchafu.

Aliwaagiza TARURA na TANROADS baada ya kukamilisha ukarabati kufanya usafi ili barabara ziwe safi na kudhibiti uharibifu unaofanywa na magari na madereva kuacha uchafu.

Meneja wa TANROADS Singida, Msama Msama, alisema wameomba fedha kwa ajili ya kufanya upanuzi Barabara Kuu ya Singida- Mwanza eneo la mlima sekenke ili kudhibiti ajali ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Elia Digha,alisema barabara ya kutoka Singida kwenda Ilongero makao makuu ya halmashauri kwa miaka mingi haitengewi fedha kwa ajili kujengwa kwa kiwango cha lami, licha ya viongozi wa kitaifa kutoka ahadi.

Digha, alisema inasikitisha kuona hata kilometa 11 ambazo zimeingizwa katika bajeti ya mwaka huo wa 2024/2025, hakuna fedha zilizotengwa kuifanyia matengenezo barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

# Manispaa yajivunia uandikishaji wanafunzi

**Na Mwandishi Wewtu,**
SINGIDA

MANISPAA ya Singida, imevuka lengo kwa kuandikisha zaidi ya wanafunzi 9,400 kuanza elimu ya awali na darasa la kwanza katika shule zake kwa kipindi cha mwaka huu.

Kaimu Ofisa Elimu Awali na Msingi Manispaa hiyo, Beno Magesa, akizungumza jana na gazeti hili alisema kuwa hadi kufikia jumatatu wiki hii uandikishaji wanafunzi wa awali ni sawa na asilimia 52.24, wakiwemo wasichana 2,325, kati ya 3,592 ya waliokusudiwa na wavulana 2112 sawa na asilimia 62.36 kati ya 3,442.

"Wanafunzi wa awali mpaka shule zinafunguliwa kuanza muhula wa masomo, Manispaa imeandikisha wanafunzi 4,237 kati ya maotokeo ya 7,034, wakiwemo wasichana 2,325 na wavulana 2,112 naamini idadi hii itaongezeka, kwa wazazi kuandikisha watoto wao, wakati masomo yakiwa yanaendelea darasani," alisema.

Kuhusu uandikishaji wanafunzi wa darasa la kwanza, Mwalimu Magesa alifafanua kuwa hadi kufikia siku ya kwanza ya muhula wa masomo, 5,251 sawa na asilimia 78.73 wameandikishwa, kati ya 6,670 ya waliokusudiwa.

Alisema kuwa kwenye idadi hiyo wapo wasichana 2,545 ambao ni sawa na asilimia 75.45, na wavulana 2,706 asilimia 82.7 ya waliokusudiwa.

Kaimu Ofisa Elimu huyo alitumia fursa hiyo kuwaomba wazazi na walezi wenye watoto ambao bado hawajaandikishwa, wahakikishe wanawapeleka katika shule zilizopo jirani na maeneo yao ili waweze kutumia haki yao ya msingi ya kupata elimu inayotolewa bure na serikali.

# Vyama vya Ushirika, SACCOS vyaagizwa kuajiri wakaguzi

**Na Paul Mabeja,**DODOMA

MRAJIS na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dk. Benson Ndiege ameviagiza Vyama Vikuu vya Ushirika nchini na vya Akiba na Mikopo(SACCOS) vikubwa nchini kuajiri na kutumia wakaguzi wa hesabu wa ndani kuongeza ufanisi.

Akizindua Kamati ya Ukaguzi ya TCDC jana jijini hapa, Dk.Ndiege, alisema kuwa wakaguzi hao ni watendaji muhimu kusaidia kubaini changamoto za ushirika na kushauri namna ya kukabiliana nazo ili kuendelea kuwa na usimamizi imara wa sekta hiyo.

Alisema serikali imeipa uzito Sekta ya Ushirika na kwamba Tume hiyo ni chombo muhimu kitachowasaidia wananchi kuwa na nguvu ya pamoja.

Alisema hadi sasa nchini kuna takriban watu milioni nane nchini wanajihusisha na vyama vya ushirika.

"Serikali imedhamiria kuimarisha ushirika kwa maslahi mapana ya nchi, Tume hii ni chombo muhimu na kinaangaliwa kwa jicho la pekee kwa maslahi makubwa ya nchi yetu," alisema Ndiega.

Alisema hadi sasa kuuna takribani vyama vya ushirika 7,000 nchini kati ya hivyo, vilivyosajiliwa kwenye mfumo wa kielektroniki 6,500.

Alisema Tume hiyo ambayo ni msimamizi wa sekta ya ushirika, inatakiwa kuwa imara na wajumbe wa kamati hiyo walioteuliwa wameingia kwa sifa na uwezo wao wa kufanya kazi ili kusaidia usimamizi wa TCDC.

"Niwaagize menejimenti kuwa kamati hii inatakiwa kupewa ushirikiano ili kufanya kazi yao vizuri kwenye taasisi nyingi, utasikia Mkaguzi wa Ndani ni wa kukaa naye chonjo kwa sababu ni mtu wa kutafuta mapungufu ili awarekebishe.

"Watu ambao wanaenda kukosea na hawafuati taratibu na hawataki kurekebishwa ni lazima ofisi yake itakuwa na changamoto, wajumbe wa kamati ya ukaguzi msitupambe lazima msimame kwenye eneo lenu mfanye kazi kwa weledi,"alisema

Awali, Mwenyekiti mstaafu wa kamati hiyo, Evance Assenga, alisema kamati yake ilishauri na kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya rasilimali, uwazi na uwajibikaji wa tume hiyo ili kuleta ufanisi kwenye sekta hiyo.

Assenga vilevile, alishauri kamati mpya kutumia kwa umakini taarifa za mkaguzi wa ndani kwa kuwa zitawasaidia kwenye ukaguzi.



# Viuatilifu tishio Nyanda za Juu Kusini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ONGEZEKO la magonjwa ya yasiyo ya kuambukizwa katika Mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini linatokana na matumizi yasiyo sahihi ya viuatilifu kwa ajili ya kilimo, imefahamika yametajwa kuwa chanzo cha ongezeko la magonjwa hayo

Kutokana na hali hiyo, Serikali imeiagiza Mamlaka ya Afya ya Mimea na Udhibiti wa Viuatilifu nchini (TPHPA) kuanza kutoa elimu ya matumizi sahihi ya viuatilifu kwa wakulima na maofisa wa serikali ili kunusuru jamii.

Mafunzo hayo yameanza kutolewa jijini Mbeya kwa siku tano yakiwahusisha wakulima, maofisa ugani na wafanyabiashara wa viuatilifu ili kuhakikisha elimu hiyo inasambaa katika maeneo yote.

Akifunga mafunzo hayo juzi Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Mbeya, Said Madito, alisema viuatilifu hivyo vina viambata vya sumu hatari kwa afya za binadamu na kuwataka maofisa hao kutoa elimu kwa kina kwa wananchi.

**"Kwa siku za karibuni magonjwa haya yameongezeka sana kutokana na matumizi holela ya viuatilifu, ninyi wataalamu ndio mnaotakiwa kuhakikisha elimu hii inawafikia wakulima wetu...**

Madito, alisema kemikali hizo ni chanzo cha magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza, ikiwemo saratani na kutaka kuongezeka kwa umakini wakati wa kutumia.

"Kwa siku za karibuni magonjwa haya yameongezeka sana kutokana na matumizi holela ya viuatilifu, ninyi wataalamu ndio mnaotakiwa kuhakikisha elimu hii inawafikia wakulima wetu, nawapongeza kwa kuanza kutoa elimu hii na naomba muendelee," alisema.

Aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuhakikisha wanapeleka elimu hiyo kwa wenzao ili wazingatie matumizi sahihi na kuepuka madhara ya viuatilifu hivyo.

Mratibu wa Mafunzo kutoka TPHPA, Jumanne Msalama, Alisema ili kukabiliana na madhara ya viuatilifu hivyo, wanahakikisha kila kinachoingizwa nchini kinasajiliwa.

Msala, alisema viuatilifu hivyo ni lazima viandikwe kwa lugha ambayo inaeleweka vizuri kwa watumiaji wakiwemo wakulima wa kawaida. Nyanda za Juu Kusini inaundwa na mikoa ya Njombe, Mbeya, Songwe, Iringa, Ruvuma na Rukwa.



Wakazi wa Kata ya Iziwa, jijini Mbeya, wakimsikiliza Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (hayupo pichani), wakati wa mkutano wake wa hadhara wa kusikiliza kero mbalimbali juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Vyanzo vya Maji Iziwa hatarini kukauka

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kata ya Iziwa ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya wamedai vyanzo vya maji viko hatarini kukauka kutokana na maofisa Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) kufyeka misitu ya asili kwenye maeneo yao.

Walitoa madai hayo juzi wakati wa mwendelezo wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Mkoa wa Mbeya ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi wa Iziwa.

Mmoja wa wakazi hao, Yoram Mkosole alisema katika eneo hilo kulikuwa na misitu mikubwa ya asili iliyokuwa inatunza vyanzo vya maji, kwa sasa imefyekwa na kupandwa miti ya mbao aina ya 'pine' ambayo sio rafiki wa maji.

Mkosole, alisema baadhi ya vyanzo vya maji vimekauka na vichache vilivyobakia kiwango cha maji yanayotoka ni kidogo na kuna uwezekano miaka kadhaa ijayo vikakauka.

"Miaka ya nyuma pale ng'ambo palikuwa na maji yanatiririka, nilikuwwa nikikaa hapa nyumbani kwangu nayasikia, kwa sasa hata ukiwa umbali wa mita 10 unasikia kwa mbali sana," alisema.

Alisema pia kuna maofisa wa serikali walikuwa wanafanya shughuli za kilimo kwenye jirani na vyanzo vya maji kabla ya kupigwa marufuku na viongozi wa mtaa. Diwani wa Iziwa, Kephas Sote, alisema ufyekaji wa miti ya asili uliofanywa na TFS ilikuwa ni maagizo ya Serikali Kuu na kwamba hauhusishi maeneo ya vyanzo vya maji kama baadhi ya wakazi hao wanadai.

Sote, alisema awali baadhi ya wakazi hao walikuwa wamepanda miti ndani ya mita 60 kutoka kwenye vyanzo hivyo na kufyekwa na kupandwa ya asili ambayo ni rafiki kwenye maeneo hayo.

Alisema TFS wamekuwa na mwendelezo wa ufyekaji huo na kupanda ya kisasa ndani ya mita 60 kutoka kingo za mito ambayo ni rafiki kwa vyanzo vya maji.

Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera, alimuagiza Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, kuunda timu kupendekeza namna sahihi ya kutunza mazingira kwenye eneo hilo ina kujadili miti inayostahili kupandwa.

Homera, alisema kamati hiyo inatakiwa kufanya kazi mwezi mmoja na kuandaa taarifa ya maamuzi ya kuiondoa miti iliyopandwa ama kupendekeza vinginevyo.

Aliwataka wakazi wa eneo hilo kutunza mazingira na vyanzo vya maji ili kuhakikisha vinakuwa endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

# Wafugaji wadaiwa kuvamia mradi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani hapa Mkoa wa Mbeya, imewaamuru wafugaji wanadaiwa kuvamia eneo la Mradi wa Kilimo cha Soya lililopo Kijiji cha Mapogoro Kata ya Chokaa kuondoka mara moja.

Amri hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Chinya, Mbarak Batenga wakati akizungumza kwenye mkutano wa hadhara na wakazi wa kijiji hicho.

Amri hiyo imekuja baada ya wakazi hao kulalamika kuwa wafugaji hao kutoka maeneo jirani, wamevamia eneo hilo na kutishia kukwama kwa utekelezaji wa mradi huo.

Walidai wafugaji hao wanadaiwa kuhamia eneo hilo kinyemela kutoka kitongoji kilichopo jirani chenye makazi ya Masiano na Mbanga.

Batenga alisisitiza kuwa wafugaji hao wanatakiwa kuondoka mara moja katika eneo hilo na kurejea kwenye maeneo yao kabla serikali haijaanza kutumia nguvu.

Alisema serikali imetoa ekari 50 kwa kila kaya na hati miliki katika eneo lililopo msitu wa kijiji ili kupisha utekelezaji wa mradi huo.

Alisema wakazi wa Mapogolo ndio wanufaika wa kwanza wa mradi huo utakapoanza utekelezaji, hivyo wanapaswa kuulinda usiendelee kuvamiwa na watu wenye nia ovu.

"Niwasihi wakazi wa vijiji hivi ambavyo mradi upo hasa vijana kujipanga kushiriki kwenye mradi huu ili kujiongezea kipato na kujikwamua kiuchumi," alisema Batenga.

Aliwasisitiza kuheshimu mpango wa matumizi bora ya ardhi baada ya kupitishwa kwenye mikutano yao ya kijiji ili kuondokana na migogoro ya ardhi na kuipa nafasi Serikali kuwaletea maendeleo

"Kupitia mpango wa matumizi bora ya ardhi tumetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 2,594 lililopo kijiji cha Mapogolo na Shoga kwa ajili ya wafugaji wa vijiji vya Masiano na Mapogolo na tunaandaa utaratibu wa kuwaletea malisho, mabwawa ya maji pamoja na kujenga majosho," alisema Batenga.

Awali wakazi hao, waliomba Serikali kutatua matatizo yaliyopo kijijini hapo ikiwemo ubovu wa barabara, upungufu wa madawati, ukosefu wa umeme, maji safi na salama.

Wakazi hao walisema hawana zahanati ya kijiji hali inayowalazimu kufuata huduma vijiji vingine. Mkuu huyo wa wilaya aliahidi kutatua matatizo hayo.

HABARI ZANZIBAR

## Wazalishaji wahamasishwa kuthibitisha bidhaa TBS

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZALISHAJI nchini wametakiwa kuthibitisha ubora wa bidhaa zao Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili kuondokana na vikwazo vya biashara kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi.

Rai hiyo ilitolewa jana na Ofisa Masoko wa TBS, Maryam Abdulaziz kwenye Maonesho ya 11 ya Kitaifa ya Biashara Zanzibar yaliyofanyika Dimani visiwani hapa.

Maryam, alisema ni muhimu kwa wazalishaji hao kuhakikisha wanatuma alama ya ubora ya TBS na kuondokana na vikwazo hivyo na kuzifanya bidhaa zao kuaminika kwenye masoko hayo na kupata wateja.

Alitoa mfano wa bidhaa inayozalishwa Zanzibar kuwa ikiwa na alama ya ubora ya Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS), haiwezi kukumbana na kikwazo cha kibiashara kwenye soko la Tanzania Bara kwa sababu ubora wake hautiliwi shaka.

Alisema bidhaa ambazo zimethibitishwa na TBS zinapopelekwa kwenye soko la Zanzibar nazo haziwezi kukumbana na vikwazo vya kibiashara kutokana na mashirika hayo kushirikiana.

"Wazalishaji ambao hawajathibitisha ubora bidhaa zao, waje TBS kwani kutawahakikishia uhakika wa masoko ndani na ya nje," alisema Maryam.

Alitoa wito kwa wajasiriamali kuchangamkia kuthibitisha ubora wa bidhaa bure kwa kuwa na barua ya utambulishi kutoka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO).

"Serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan inatambua mchango wa wajasiriamali katika kukuza uchumi, ndiyo maana inabeba gharama zote za wajasiriamali kuthibitishiwa bidhaa zao bure," alisema.

Aliwataka wananchi kuwa mabalozi wa kuhamasisha matumizi ya bidhaa zenye ubora na kuepuka matumizi ya bidhaa zilizokwisha muda wake wa matumizi.

Aliwashauri kujenga utamaduni wa kusoma taarifa zinazokuwa kwenye vifungashio vya bidhaa ili kubaini kama hazijaisha muda wake wa matumizi na kama zimethitishwa na TBS.

Aliwataka kutoa taarifa za bidhaa ambazo muda wake umwekwisha na ambazo hazina alama ya ubora ofisi ya TBS.

# Utafiti magonjwa ya mifugo kufanyika Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban amesema serikali inajenga maabara ya kisasa ya utafiti wa magonjwa ya mifugo nchini ili kupunguza gharama kwa kupeleka nje ya nchi.

Shaaban, aliyasema hayo wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa maabara ya utafiti wa magonjwa ya wanyama katika Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar (ZALIRI) iliyopo Dole Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja.

Alisema pamoja na mafanikio yaliyopo katika sekta ya mifugo, wafugaji wa Zanzibar wanaendelea kuathirika na uzalishaji mdogo kutokana na uhaba wa malisho na chakula kwa mifugo.

"Kutokana na changamoto hiyo, maabara hii inapaswa kuwa nguzo muhimu kuinua sekta ya mifugo kwa kuimarisha utafiti mbayo ni sehemu muhimu ya chakula cha binadamu", alisema Shaaban.

**"Kutokana na changamoto hiyo, maabara hii inapaswa kuwa nguzo muhimu kuinua sekta ya mifugo kwa kuimarisha utafiti mbayo ni sehemu muhimu ya chakula..."**

Alisema ujenzi wa maabara hiyo utaongeza uzalishaji wa mazao ya mifugo na kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

Alisisitiza kuwa serikali inaendelea kubuni mikakati ya kujenga viwanda vya vyakula ikiwemo vitokanavyo na mifugo, hivyo maabara hiyo itatumika kufanya tafiti zenye ubora na kuwaletea wananchi maendeleo ya kisayansi kwa mifugo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Ali Khamis Juma, alisema ujenzi wa maabara hiyo unakwenda sambamba na wa banda la utafiti wa kondoo.

Juma, alisema fedha za ujenzi huo zimetolewa na serikali na washirika wa maendeleo.

Alisema ujenzi huo utafanyika kwa awamu mbili, ya kwanza ya maabara ya utafiti wa vinasaba vya magonjwa hayo ya mifugo.

"Maabara hii itahusika na utambuzi wa aina ya maradhi ya wanyama," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar (ZALIRI), Dk. Talib Saleh Suleiman, alisema taasisi hiyo ina malengo ya kuendeleza mifugo na kufanya utafiti wa malisho na lishe kwa wanyama.

Suleiman, alitaja tafiti nyingine kuwa ni za magonjwa ya wanyama, jamii na uchumi. Aliipongeza serikali kwa kutoa fedha za ujenzi huo na kuondokana na gharama za kupeleka sampuli za mifugo iliyokumbwa na magonjwa kufanyiwa uchunguzi nchi za nje.




Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Mudrik Ramadhan Soraga (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, Unguja jana, kuhusu tamasha la pili la utalii wa biashara na uwekezaji Zanzibar linalotarajiwa kufanyika visiwani humo mwezi Mei mwaka huu.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yaendelea kusaka wawekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) inaendelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji ili wawekezaji wengi zaidi wawekeze nchini.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana katika mazungumzo na Balozi wa Tanzania nchini Nigeria, Balozi Celestine Kakele aliyefika Ikulu kujitambulisha na kumuaga.

Alisema kuna fursa nyingi ambazo nchi hizo zinaweza kushirikiana kiuchumi na uwekezaji ambazo bado hazijafanyiwa kazi. Alimtaka Balozi Kakele kutilia mkazo utalii na uwekezaji ambayo ndio chachu ya uchumi wa Zanzibar kwa sasa.

Dk. Mwinyo, alisema Serikali inaendelea kuimarisha sekta ya uwekezaji kwa kuondoa vikwazo vinavyozorotesha ushirikiano baina ya nchi hizo.

Eneo jingine ambalo Dk. Mwinyi alilisisitiza ni sekta ya biashara ambayo alisema ikifanyika vizuri nchi hizo zinaweza kunufaika zaidi.

Alisema jingine analipaswa kutilia mkazo ni kutangaza bidhaa za Afrika Mashariki ili zipate sokon nje ya nchi hizo.

Mwinyi, alisema nchi hizo zinaweza kuwa na biasahara kubwa kwa kuuziana bidhaa za ndani na kutoa mfano wa mazao ya baharini na dagaa yanayopatikana kwa wingi Zanzibar.

Kwa upande wake, Balozi Kakele, alisema Nigeria ni nchi kubwa na yenye fursa nyingi za kiuchumi na uwekezaji.

Alisema Tanzania ikiwemo Zanzibar inaweza kunufaika nazo na kushauri kuimarishwa kwa upatikanaji wa 'Viza' baina ya nchi hizo.



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Pwani, Boniphace Jacob (katikati) na Ofisa wa Masuala ya Haki za Binadamu, Godlisten Malisa (kulia), wakiwa na wakili wao, Hekima Mwasipo, wakitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kesi inayowakabili ya kuchapisha taarifa za uongo katika mitandao ya kijamii kuahirishwa kutokana na shahidi kutofika mahakamani na nyingine hakimu kutokuwapo. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# TAKUKURU, TRA bega kwa bega kusimamia kikamilifu ulipaji kodi

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Crispin Chalamila, amesema taasisi hiyo itaendelea kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika kuhakikisha kodi ya serikali inakusanywa kikamilifu.

Aliyasema hayo juzi katika mazungumzo na Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Mwenda, alipomtembelea ofisini kwake, jijini Dar es Salaam.

Chalamila alisema licha ya kushirikiana na TRA katika kuhakikisha kodi yote inakusanywa, pia watahakikisha inatumika kwa ajili ya matumizi yaliyopangwa na serikali.

Alisema TAKUKURU na TRA ni taasisi muhimu kwa ustawi wa nchi, hivyo ushirikiano wao utakuwa na tija katika kuisaidia serikali kuleta maendeleo kwa wananchi.

Alisema maendeleo wanayoyaona nchini ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo ya elimu, afya na miundombinu ni matokeo ya wazi ya kodi zinazokusanywa na TRA.

Chalamila alisema TRA inapaswa kuungwa mkono na kuielimisha jamii kutambua hicho ni chombo chao.

Kamishna Mkuu wa TRA, Mwenda, aliishukuru TAKUKURU kwa ushirikiano wanaoonyesha kila panapohitajika katika kuhakikisha majukumu ya mamlaka hiyo hayakwami.

Alisema TRA inafanya kazi kwa karibu na TAKUKURU katika kuhakikisha hakuna kodi inayokwepa huku wakiziba mianya ya rushwa na ukwepaji na kuchukua hatua stahiki kwa wanaobainika kukutwa na hatia za rushwa na wanaokwepa.

"Tunaishukuru sana TAKUKURU kwa ushirikiano wao wa muda wote katika kuhakikisha kodi yote inakusanywa kwa ajili ya maendeleo ya taifa na kuweka msukumo katika usimamizi wa matumizi yaliyo sahihi," alisema Kamishna Mkuu Mwenda.

# Ng'ombe 478,974, mbuzi 49,848 wapewa chanjo

**Na Jumbe Ismailly,** MANYONI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Manyoni mkoani Singida imetoa chanjo ya magonjwa ya mifugo kwa ng'ombe 478,974 pamoja na mbuzi 49,848 katika kipindi cha mwaka 2019 hadi 2022.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Anastazia Tutuba alitoa takwimu hizo alipokuwa akitoa taarifa za utoaji chanjo za magonjwa mbalimbali ya mifugo katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

Alisema katika kipindi cha miaka minne iliyopita ng'ombe 139,411 walipatiwa chanjo ya ugonjwa wa kimeta, kati ya hao 104,108 walichanjwa chanjo ya ugonjwa wa chambavu, huku 146,204 walipatiwa chanjo wa mapele ngozi.

Alisema ng'ombe 89,251 na mbuzi 49,848 walipatiwa chanjo ya ugonjwa wa homa ya mapafu.

Hata hivyo, alisisitiza kwamba kila mfugaji aliyepeleka mifugo katika chanjo hiyo alitozwa gharama kulingana na tozo elekezi zilizowekwa na Wizara ya Mifugo na kwamba kabla na baada ya kutolewa kwa chanjo hiyo hakuna madhara yoyote yaliyotokea.

Kaimu Mkuu wa Mawasiliano Serikalini katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Frank Samatha, aliweka alisema magonjwa yanayotolewa chanjo husababishwa na virusi pamoja na bakteria.

Kadhalika, alizitaja faida za chanjo hizo kuwa ni kuongeza uzalishaji wa nyama pamoja na maziwa.

Alisema kabla ya kutolewa kwa chanjo ya ugonjwa wa homa ya mapafu kwa ng'ombe pamoja na mbuzi umekuwa ukisababisha vifo vingi kwa mifugo katika kipindi cha mwaka 2019 na 2020.

Alizitaja faida zingine ni kupunguza vifo, kuongeza kipato cha mfugaji na taifa, kukidhi soko la kimataifa la mazao ya mifugo kama vile nyama na maziwa.

Hata hivyo, alizitaja baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utoaji wa chanjo kuwa ni baadhi ya wafugaji kukaidi kupeleka mifugo kupatiwa chanjo kutokana na imani potofu.

Alitaja sababu nyingine ni jiografia ya wilaya hiyo baadhi ya maeneo yamekuwa hayapitiki kirahisi.

Alisema changamoto zingine ni baadhi ya wafugaji kukaa kwenye maeneo ya mbali ambayo yana mapori kutofikika, baadhi ya wafugaji kuficha mifugo yao ili isipate chanjo pamoja na uhaba wa vitendea kazi.

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 28095/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late LAZARO KISSY MANDARA of Miyuji Proper Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY KISSY LAZARO MANDARA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 13 Day of 01, 2025
Date at Dodoma this 28TH Day of OCTOBER, 2024.

PETITIONER
**Presented for filling this 19 day of 11,2024**

RESIDENT MAGISTRATE

---

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**LUKUNGU INVESTMENT CO. LIMITED** inatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 620 CCP – KINGLIONE** yenye Chassis namba **BPKM3H2TLPK024532.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/IRI/IRI/881/2025.**

---

**KUPOTEA KWA KADI YA GUTA**

**LEONARD MWAJOMBE** anatangaza kupotelewa na kadi ya GUTA yenye namba za usajili **MC 909 DDU – SINORY** yenye Chassis namba **LZSHDNZG9M8008477.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/IRI/IRI/391/2025.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 29346/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late DICKSON NELSON SEMANGO of Mkuyuni-Kikuyu Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ODELA EZEKIEL HEBUYE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 25 Day of January, 2025

Date at Dodoma this 14TH Day of November, 2024.

PETITIONER
**Presented for filling this 22 day of November, 2024**

RESIDENT MAGISTRATE

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOPO SONGEA**

**MAOMBI NAMBA 89/2024**

**SWALEHE KASANDA.............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**AMINA MILANZI..................MJIBU MAOMBI**

**WITO KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi unataarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako. Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako au wote pamoja siku ya tarehe 17/1/2025 saa 6:00 mchana. Shauri linakuja kwa ajili ya hukumu.
Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kutoa hukumu katika shauri bila kujali uwepo wako.
Imetolewa leo name na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 13/01/2025.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
SONGEA

---

**KUPOTEA KWA KADI YA TRACTOR**

**AUGUSTINO FRANCES KAOGO** anatangaza kupotelewa na kadi ya Tractor yenye namba za usajili **T 488 EBA.** Chassis namba **YS2R6X2001256449.** Engine namba **0065546419.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **PHQ/NJO/NJO/355/2025.**

---

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI NA BAJAJI**

**BAKARI TWAHA RENO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 175 ABF - ASIA COMBI.** Kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 379 BHZ – TVS.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/7896/2025.**

---

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**DIWANI SAIDI KIMWERI** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T.236 CAC.** Yeyote akatayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MSS/RB/45/2024.**

---

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**GEORGE ROBERT TAWE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI **T 413 DTE** ILIYOPOTEA KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/941/2025.**

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MARATHI NA.30502 YA MWAKA 2024.**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**

**BAHADUR JAMAL ALIBHAI UKANI@BAHADUR ALIBHAI**

**NA**

**HAIDERALI JAMAL ALIBHAI UKANI@HAIDER ALIBHAI AND FAHAR ALIBHAI SHAMJI..............................................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa waombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 13 FEBRUARI, 2025, Saa 10:00 Asubuhi. Siku ambayo shauri hili limepangwa kusikilizwa Mbele ya Mhe. Jaji S. MWAIPOPO
Imesainiwa Dar es Salaam, leo tarehe 07th Mwezi wa JANUARI, 2025

NAIBU MSAJILI

HABARI KIMATAIFA

## Wachimbaji madini 26 waokolewa mgodini

**CAPETOWN,** Afrika Kusini

ZAIDI ya wachimbaji madini haramu 26, wameokolewa na miili ya watu kumi kuondolewa ndani ya mgodi nchini Afrika Kusini.

Operesheni za uokozi zilianza tena jana kwa ajili ya kuwafikia watu wengine ambao wamekataa kutoka kwa hiari ndani ya mgodi huo uliotelekezwa.

Kiongozi wa eneo hilo, Johannes Qankase, amesema wachimbaji hao waliookolewa walikuwa katika hali mbaya kutokana na kuwa na upungufu wa maji mwilini.

Alisema wengi wao walipelekwa hospitalini wakati wawili wanaaminika kushikiliwa na polisi. Maofisa wa serikali walitarajiwa kulitembelea eneo hilo la mgodi wakati shughuli ya uokozi zikiendelea.

Operesheni hiyo inafuatia sakata la kuhakikisha wachimbaji hao wanatoka kwa hiari lilodumu kwa wiki kadhaa kushindikana.

Polisi wa nchi hiyo wanatuhumiwa kwa kujaribu kuwalazimisha wachimbaji hao kujitokeza nje kwa kuwazuia raia kuacha kuwateremshia chakula na maji ndani ya mgodi.

Haijulikani wazi ndani ya mgodi huo kuna watu wangapi waliobaki. Lakini serikali ilisema jana kuwa zaidi ya watu 1,000 wanaohushwa katika uchimbaji haramu wa madini katika eneo hilo wametoka mgodini na kukamatwa mpaka sasa. **DW**

**Operesheni hiyo inafuatia sakata la kuhakikisha wachimbaji hao wanatoka kwa hiari lilodumu kwa wiki kadhaa kushindikana.**



Wapalestina wakiwabeba watu waliojeruhiwa ili kuwapeleka hospitali kufuatia shambulio la anga la Israel kwenye jengo la makazi mjini Khan Younes jana.**PICHA: GETTY IMAGES**

# Israel, Hamas kumaliza vita wakati wowote

**TEL AVIV,** Israel

KUNDI la Hamas limekubali rasimu ya makubaliano ya kusitisha vita katika ukanda wa Gaza na kuachiliwa huru kwa mateka wa Israel.

Hayo yalielezwa na maofisa wawili wanaohusika katika mazungumzo ya usitishaji vita yanayofanyika mjini Doha, nchini Qatar.

Wapatanishi kutoka Marekani na mataifa ya Kiarabu walisema Israel na kundi la Hamas wako karibu kufikia makubaliano, hatua ambayo itaashiria kumalizika kwa vita vilivyodumu zaidi ya miezi 15.

Shirika la Habari la Associated Press, lilipata nakala ya makubaliano yaliyopendekezwa ya kusitisha mapigano, huku maofisa wa Misri na Hamas wakithibitisha uhalali wa nakala hiyo.

Ofisa wa Israel alifahamisha kuwa kuna maendeleo makubwa kuelekea kufikia makubaliano hayo, japo maelezo ya mwisho bado yanafanyiwa kazi.

Waziri wa mambo ya nje wa Marekani Antony Blinken, anaamini wanakaribia kufikia makubaliano ya kusitisha mapigano na kuongeza kwamba, uamuzi huo uko mikononi mwa Hamas.

"Tuko karibu sana. Karibu zaidi kuliko wakati wowote ule, taarifa rasmi inaweza kutolewa aidha ndani ya saa chache au siku." Alisema.

Marekani, Misri na Qatar zimekuwa katika mstari wa mbele kuongoza juhudi za kufikia makubaliano ya kusitisha mapigano na kuachiliwa kwa mateka.

Inaripotiwa kwamba takriban watu 100 bado wanashikiliwa mateka ndani ya Gaza, huku jeshi la Israel likiamini kuwa watu wapatao 33 tayari wamekufa.

Makubaliano yoyote yatakayofikiwa yanatarajiwa kusitisha mapigano na kufungua fursa ya matumaini ya kupunguza vita vikali na vya na uharibifu ambavyo Israel na Hamas wamewahi kupigana.

Mgogoro huo umevuruga eneo zima la Mashariki ya Kati na kusababisha maandamano katika sehemu mbalimbali duniani.

Makubaliano hayo pia yataleta nafuu ndani ya Ukanda wa Gaza, ambao umeharibiwa vibaya kufuatia oparesheni ya kijeshi ya Israel.

Mpango huo utahitaji idhini kutoka kwa baraza maalum la usalama la Waziri Mkuu, Benjamin Netanyau na kisha baadaye baraza lake zima la mawaziri.

Mabaraza yote hayo yanatawaliwa na washirika wa Netanyahu na kwa kiasi kikubwa, yanatarajiwa kuunga mkono mapendekezo yoyote yatakayowasilishwa kwao.

Kuna kila dalili kuwa makubaliano hayo yataafikiwa kabla ya kuapishwa kwa Rais mteule wa Marekani Donald Trump, Januari 20, ambaye mjumbe wake wa Mashariki ya Kati pia amejiunga kwenye mazungumzo hayo.

Hamas iilieleza katika taarifa kwamba mazungumzo yamefikia hatua ya mwisho.

01:57

Wakati huo huo, maelfu ya watu walikusanyika mjini Tel Aviv kuunga mkono makubaliano ya kusitisha mapigano ambayo wamekuwa wakiyatamani kwa muda mrefu.

Mateka mmoja aliyeachiliwa kutoka Gaza Moran Stella Yanai alisema suala hilo sio suala la siasa au mikakati. Ni kuhusu utu na imani ya pamoja kwamba hakuna mtu yeyote anayepaswa kuachwa gizani.

Hata hivyo mjini Jerusalem, mamia ya watu wenye misimamo mikali waliandamana kupinga makubaliano hayo. Baadhi wakiimba nyimbo na kueleza upinzani wao kwamba, Israel haipaswi kuingia makubaliano na shetani, wakimaanisha kundi la Hamas.

**DW**

# Hatimaye Rais Korea Kusini akamatwa

**SEOUL,** Korea Kusini

HATIMAYE Rais wa Korea Kusini aliyeondoshwa madarakani, Yoon Suk Yeol amekamatwa, baada ya wiki kadhaa ya mvutano kuhusu uhalali wa kuchukuliwa hatua hiyo.

Kwa mujibu wa mamlaka husika, kiongozi huyo alikamatwa jana kwa ajili kuchunguzwa kutokana na hatua yake ya kuamrisha sheria ya kijeshi nchini humo.

Yoon ndiye rais wa kwanza aliye madarakani nchini humo kukamatwa.

Mtandao wa Yanhap, ilisema timu ya wachunguzi walifanikiwa kuingia makazi ya rais kwa kutumia ngazi.

Awali, wachunguzi hao walizuiliwa mapema na wabunge wa chama tawala na mawakili wa Yoon kwenye lango la kuingilia, pamoja na kizuizi cha magari kilichowekwa.

Lakini baadhi ya wachunguzi waliripotiwa kufanikiwa kufikia eneo hilo kupitia njia iliyo karibu ya kupanda mlima.

Na hivyo ndivyo wachunguzi hao walivyofanikiwa kuingia nyumbani kwa rais, mamlaka imethibitisha.

Waandamanaji walionekana mara kwa mara walikita kambi katika makazi ya rais katika kipindi cha wiki chache zilizopita na asubuhi ya jana umati huo ulijitokeza tena wakitazama jinsi wachunguzi wanavyoendesha jaribio lao la pili la kumkamata Yoon.

Katika taarifa ya video, Rais Yoon alisema amekubali kufika mbele ya Ofisi ya Uchunguzi wa Ufisadi, ambayo inaongoza kesi dhidi yake.

"Niliamua kufika mbele ya CIO, ingawa ni uchunguzi usio halali, ili kuzuia umwagaji wa damu mbaya," alisema.

Aliongeza "Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba ninaidhinisha uchunguzi wao."

Katika video hiyo fupi iliyo chini ya dakika tatu, alisema kuwa utawala wa sheria nchini humo umevunjwa, na kwamba sio vyombo vinavyomchunguza, wala mahakama zinazowapa hati ya kukamatwa, walikuwa na uwezo wa kufanya hivyo.

Alimalizia kwa kusema japo siku hizo ni za giza, lakini mustakabali wa taifa hilo una matumaini. **BBC**

# TABORA UNITED YAONGEZA NGUVU, YASAJILI KIPA MPYA

**Na Adam Fungamwango**

HAWATAKI mchezo, ikiwa imeonyesha ushindani katika mzunguko wa kwanza, uongozi wa Tabora United umetangaza kumsajili golikipa, Jean Noel Amonone, ambaye ni raia ya Gabon.

Klabu hiyo imemtangaza kipa huyo baada ya kukamilisha mazungumzo na kipa huyo ili kukiongezea nguvu kikosi chao.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana, imesema imemsajili Amonone kutoka Klabu ya AS Arta Solar ya Djibouti.

"Tumemsajili kipa kutoka Gabon katika kuimarisha kikosi chetu kuelekea mzunguko wa pili, tunaamini ataongeza ubora katika kikosi chetu," ilisema sehemu ya taarifa ya klabu hiyo.

Kipa huyo anakwenda kuungana na makipa wengine Haroun Mandanda, pamoja na Fikirini Bakari kutoka Singida Black Stars, lakini alikuwa akiichezea Fountain Gate kwa mkopo.

Kipa huyo amepishana na Hussein Masalanga, aliyekuwa akiichezea Tabora United kwa mkopo akitokea Singida Black Stars.

Ofisa Habari wa Singida Black Stars, Hussein Massanza, amekiri kumjeresha kundini Masalanga baada ya kuichezea Tabora United kwa muda wa miezi sita akieleza sababu ni kiwango bora alichokionyesha katika mechi za mzunguko wa kwanza.

Kutokana na hali hiyo, Singida Black Stars wameamua kumpeleka Fikirini katika kikosi cha Tabora United, kwa kile kilichodaiwa kutoridhishwa na kiwango alichokionyesha katika mchezo dhidi ya Pamba Jiji iliyochezwa Novemba 5, mwaka jana kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa ulioko Babati mkoani, Manyara, akiigharimu timu yake kufungwa mabao 3-1.

Kipa huyo anakuwa ni usajili wa pili kutangazwa na Tabora United, ambapo siku mbili zilizopita ilikamilisha mchakato wa kumnasa kiungo mkabaji raia wa Cameroon, Cedric Martial Zamba, kutoka timu ya Touarga ya Morocco.

Tabora United ambayo katika mechi za awali za Ligi Kuu Tanzania Bara haikuwa na matokeo chanya, sasa imeonekana ni tishio mara baada ya ujio wa Kocha Kiazayidi raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, akichukua nafasi ya Mkenya, Francis Kimanzi.

Hadi inamaliza mzunguko wa kwanza, inashika nafasi ya tano ikiwa na pointi 25 kwa michezo 15 iliyocheza, ikishinda michezo saba, sare nne ya kupoteza minne, ikifunga mabao 19 na kufungwa 19 pia.



Mwanamuziki wa nyimbo za injili, Rehema Simfukwe (kulia) na mumewe, Isaya Lyimo (kushoto), wakijiandaa kukata keki ili kusherehekea kumbukizi ya kuzaliwa kwa binti yao, Dorcas (hayupo pichani), aliyetimiza umri wa miaka sita ambaye ana changamoto ya mtindio wa ubongo. Simfukwe amefungua Kituo cha Dorcas Homecare, ambacho kitalea bure watoto wenye changamoto hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waganda kicheko michuano GIFT

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Boni Consilli Girls kutoka Uganda, David Bbale, amewapongeza wachezaji wake kwa kuonyesha kiwango kizuri katika mchezo wao Mashindano ya Wasichana ya CAF U-17 GIFT dhidi ya Aigle Noir ya Burundi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi.

Akizungumza na gazeti hili, Bbale alisema licha ya mechi hiyo kumalizika kwa sare ya bao 1-1, wachezaji wake walipata nafasi nyingi za wazi isipokuwa walishindwa kuzitumia.

"Wachezaji wangu walipata nafasi nyingi za wazi isipokuwa walishindwa kuzitumia na kufanya matokeo ya mwisho kuwa sare ya bao 1-1," alisema Bbale.

Kocha huyo aliongeza kupitia mashindano hayo wachezaji wake wamejifunza vitu vingi ambavyo vitaweza kuwasaidia katika michuano inayofuata.

Naye Kocha Mkuu wa Aigle Noir, Jean Ndikumana, alisema kipindi cha kwanza timu yake ilishindwa kufanya vizuri kutokana na kukosa umakini.

Ndikumana alisema baada ya dakika 45 za kipindi cha kwanza kumalizika alitumia muda wa mapumzuki kuzungumza na wachezaji wake ambao walifuata maelekezo yaliyopelekea kupata goli la kusawazisha walipoingia kipindi cha pili.

"Baada ya kwenda mapumziko niliwapa maelekezo wachezaji wangu ambayo waliyafanyia kazi na kupata goli la kusawazisha, walinifurahisha kwa kufanya kile nilichowaambia," alisema Ndikumana.

# Mashujaa FC yatangaza kumnasa Lyanga

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha dogo la usajili limefungwa jana usiku, Klabu ya Mashujaa imefanikiwa kukamilisha usajili wa straika mkongwe nchini, Danny Lyanga.

Straika huyo amejiunga na Mashujaa akitokea JKT Tanzania ambapo ameichezea kwa nusu msimu.

Tayari mchezaji huyo ameshajiunga na kambi ya Mashujaa tayari ili kuanza mazoezi kwa ajili ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Karibu, Lyanga kwenye familia ya kishujaa. Aliyekuwa mshambuliaji wa JKT Tanzania amejiunga rasmi na klabu yetu ya Mashujaa ya Kigoma. Tayari ameripoti kambini na ameanza mazoezi," ilisema taarifa rasmi ya klabu hiyo iliyotolewa jana.

Lyanga anakuwa usajili wa kwanza kwa klabu hiyo kutangazwa rasmi, ikiwa ni mahitaji wa benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Mohamed Abdallah 'Bares', yenye lengo la kukiboresha kikosi chake.

Lyanga ni mmoja kati ya wachezaji waliozichezea klabu mbalimbali hapa nchini, akianza na Coastal Union mwaka 2016, kabla ya kujiunga na Simba, ambapo mwaka mmoja baadaye alitimkia Fanja ya Oman.

Baada ya hapo alirejea nchini na kuichezea Azam FC, kati ya mwaka 2018 na 2019 alipoichezea Ruvu Shooting na kuelekea Geita Gold mpaka 2023 alipokwenda JKT Tanzania.

Wakati huo huo, Mashujaa imesema mchezaji wake, Ismail Mgunda bado ataendelea kuichezea klabu hiyo na kuwataka mashabiki kupuuza taarifa anaenda kujiunga na AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

"Mchezaji huyu bado ni mali ya Mashujaa, ana mkataba wa kuitumikia kwa mwaka mmoja na nusu, hivyo kwa sasa hatuwezi kumtoa kwa timu yoyote ile," ilisema taarifa hiyo.



Mgunda ambaye amekuwa katika kiwango kizuri msimu huu, alijiunga na Mashujaa akitokea Singida Black Stars.

Kabla ya hapo, Mgunda aliwahi kuzichezea timu za Ruvu Shooting na Jomo Cosmos ya Afrika Kusini.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CHELSEA WAWEKA BEI KUBWA

CHELSEA itataka ada ya pauni milioni 65 kwa mshambuliaji Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 27, huku Bayern Munich ikimtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa anayeripotiwa kutokuwa na furaha Stamford Bridge. (***Athletic***)

### ZUBIMENDI MAMBO SAFI ARSENAL

ARSENAL ipo kwenye mazungumzo kumnunua kiungo wa kati wa Real Sociedad na Hispania, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 25, kwa mkataba wa pauni milioni 51 msimu wa joto. (***Mail***)

### RASHFORD AITAKA BARCELONA

MARCUS Rashford mwenye umri wa miaka 27 anataka kuhamia Barcelona kabla ya chaguo jingine mwezi huu iwapo mshambuliaji huyo ataondoka Manchester United. (***Sport***)

### MUANI MBIONI KUTUA JUVENTUS

JUVENTUS inakaribia kumnunua mshambuliaji wa Paris St-Germain na timu ya taifa ya Ufaransa mwenye umri wa miaka 26, Randal Kolo Muani. (***Gazzetta dello Sport***)

### MESSI KURUDI BARCELONA

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 37, anaweza kujiunga tena na Barcelona kwa mkopo mara tu atakaposaini mkataba mpya na Inter Miami. (***El Nacional***)

### NUNEZ AWEKEWA NGUMU

LIVERPOOL imekataa dau la pauni milioni 70 kutoka kwa klabu ya Saudi Arabia ya Al-Hilal kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji wa Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 25. (***Anfield Watch***)

### SILVA KWA MKOPO WEST HAM

KLABU ya West Ham ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Ureno, Andre Silva mwenye umri wa miaka 29 kwa mkopo kutoka RB Leipzig kwa kipindi kilichosalia cha msimu huu. (***Guardian***)

### JHON DURAN HAENDI POPOTE

ASTON Villa imekataa dau la pauni milioni 40 kutoka kwa West Ham kumnunua mshambuliaji wa Colombia, Jhon Duran mwenye umri wa miaka 21. (***Sportsport***)

### FLAMENGO YAMTAKA JORGINHO

KIUNGO wa kati wa Arsenal na Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 33 ambaye mkataba wake unaisha msimu wa majira ya joto, anatakiwa na klabu ya Brazil, Flamengo. (***Sky Sports***)

### DISASI KUONDOKA CHELSEA

MLINZI wa kati wa Ufaransa, Axel Disasi mwenye umri wa miaka 26, ndiye mchezaji wa hivi karibuni zaidi ambaye anaweza kuondoka Chelsea kutokana na kukosa muda wa kucheza. (***Mirror***)

### TOMORI AWANIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United imekuwa ikimfuatilia mlinzi wa kati wa AC Milan na England, Fikayo Tomori mwenye umri wa miaka 27. (***Football Insider***)

### LOUIS BARRY ATAKIWA CELTIC

CELTIC ni moja ya klabu kadhaa zinazotaka kumsajili mshambuliaji wa Aston Villa, Louie Barry mwenye umri wa miaka 21 kwa mkopo, lakini timu hiyo ya Ligi Kuu England inatathmini chaguo lao. (***Sky Sports***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ZUBIMENDI AKARIBIA KUSAJILIWA ARSENAL

**LONDON,** England

ARSENAL inatarajia kushinda katika mbio za kuwania kumsajili kiungo wa kati wa Real Sociedad, Martin Zubimendi, huku dili la pauni milioni 51 likisubiriwa kutimia kwa mujibu wa ripoti.

Zubimendi mwenye kipaji cha ufundi ambaye anafanya anakiwasha kwenye kazi kwenye safu ya kiungo ya Real Sociedad aliikataa Liverpool msimu uliopita wa majira ya joto akiamua kubakia katika klabu yake ya utotoni ili kujiendeleza kama mchezaji.

**Baada ya miezi sita zaidi ya soka la kuvutia katika ligi kuu ya Hispania, Zubimendi sasa yuko tayari kuondoka.**

Liverpool waliendelea kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 na Manchester City walikuwa wamemtambua kama mbadala wa

**Nyota huyo awali alikataa dili la kujiunga na Liverpool, lakini kwa sasa yupo mbioni ku...**

Rodri.

Hata Real Madrid walijiunga katika orodha ya timu zinazomuhitaji, lakini Arsenal inaonekana kuwashinda wapinzani hao.

Washikabunduki hao wamekubali kuanzisha kifungu cha kutolewa cha pauni milioni 51 katika mkataba wa Zubimendi, hatua hiyo "imekamilika" kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Licha ya Arsenal kutaka kumleta Mhispania huyo London mwezi huu, Real Sociedad imesisitiza kumbakisha nyota wao huyo hadi msimu uajo.

Wengi wanaweza kuhoji kwamba kiungo mpya hapaswi kuwa kipaumbele cha uhamisho wa Arsenal, lakini Gabriel Jesus anaweza kuwa nje ya uwanja kwa muda wote uliosalia wa msimu huu kutokana na jeraha la goti alilopata wakati wa mchezo wa Kombe la FA wikendi iliyopita dhidi ya Manchester United, na kuongeza kukosekana kwa washambuliaji wenzake Bukayo Saka na Ethan Nwaneri.

Arteta alikiri kwamba klabu "inaingia sokoni ili kuboresha kikosi", lakini wanazuiliwa na vikwazo zaidi ya kawaida vya dirisha la majira ya baridi.

Huku Neto na Raheem Sterling wakiwa tayari wako kwa mkopo, Arsenal haiwezi kusajili tena wachezaji wa mkopo kutoka klabu za Ligi Kuu England kwa muda wote uliosalia.



# SLOT: SIKUTAKA ZAIDI KUTOKA KWA WACHEZAJI

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Arne Slot amesema "sikuhitaji zaidi" kutoka kwa wachezaji wake dhidi ya wanaowania ubingwa wa Ligi Kuu England Nottingham Forest, kwani aliridhishwa na kiwango walichokionesha.

Forest waliwabana vinara hao wa ligi hiyo kwa sare ya 1-1 kweye Uwanja wa The City Ground Jumanne usiku, huku Diogo Jota akifunga bao kwa kichwa kipindi cha pili akisawazisha lile la mapema la Chris Wood.

Liverpool walionekana kuwa mbali na ubora wao dhidi ya kikosi cha kocha Nuno Espirito Santo, lakini wamebakia na pointi sita kileleni mwa msimamo wa Ligi, wakiwa na mchezo mkononi dhidi ya timu nyingi zilizo chini yao, na Slot aliwapongeza wachezaji wake kwa juhudi baada ya mechi.

"Nisingeweza kutaka zaidi leo (juzi)," alisema kocha huyo raia wa Uholanzi baada ya mchezo huo.

"Nadhani watu wengi wangezungumza vyema kuhusu kipindi cha pili lakini ukicheza kwenye uwanja huu dhidi ya timu hii ambayo iko katika hali nzuri, ni vigumu kuruhusu nafasi katika kila mchezo.

"Tuliruhusu shambulizi moja pekee la kaunta leo (juzi) na wakaitumia vizuri."

Aliongeza, "Kuwa nyuma kwa 1-0 ni ngumu sana kufunga dhidi ya timu hii, sio kile tulichotaka.

Tulitaka pointi tatu, lakini ninachotaka na kile ambacho mashabiki na wachezaji wanapaswa kutaka wakati mwingine hakitimii."

Ulikuwa mchezo wa kuvutia kutoka kwa Forest, ingawa kipa Mats Selz alilazimika kuokoa hatari kadhaa katika kipindi cha pili kutoka kwa Jota na Cody Gakpo.

Alipoulizwa kama anaona Forest ni washindani wa kweli wa taji, Slot alisema, "Sidhani wapo hapa kwa sababu ya bahati. Kwa kila timu, ni vigumu kucheza dhidi yao.

Tayari wamekuwa na mechi ngumu za ugenini, dhidi ya Manchester United, Man City, Arsenal na sisi.

"Hiyo inakuonesha kuwa wao ni timu ambayo inaweza kushindana hadi mwisho."

# Jinamizi la sare laiandama Juventus

**TURIN,** Italia

KOCHA wa Juventus, Thiago Motta ameelezea kufadhaika kwake baada ya sare ya timu yake dhidi ya Atalanta Jumanne usiku, akikiri kwamba ingawa hawajapoteza, lakini idadi yao ya sare inayoongezeka ina maana kwamba timu hiyo ya Turin haifikii matarajio yao.



Juve ambao wapo nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Italia, Serie A, walisawazishwa tena Jumanne, safari hii kwa Atalanta ambapo bao la Pierre Kalulu lilifutwa na Mateo Retegui.

Motta alikiri kwamba licha ya Juve kutofungwa msimu huu, idadi ya sare ina maana kwamba matokeo yao hayatoshi kwa klabu huku kikosi chake sasa kikiwa kimetoka sare katika mechi 13 na kikiwa na pointi 34 ambapo ni 15 pungufu kuliko msimu uliopita.

"Ni wazi kwamba hatuwezi kufurahishwa na matokeo, tunaenda uwanjani kushinda. Tulicheza vizuri, tulitengeneza mazingira ya kuvutia, lakini hatukuwa wa kutosha kufunga," Motta aliwaambia waandishi wa habari.

"Ni kweli tumetoka sare nyingi msimu huu na hatujafurahishwa na hilo, hatuwezi kufurahishwa na sare.

"Hata hivyo, wachezaji walifanya vyema. Lazima nitambue juhudi na utendaji.

"Sasa tuna mechi muhimu dhidi ya timu kubwa, tunahitaji kupona vyema," aliongeza, akimaanisha ziara ya kwenda kucheza na AC Milan iliyo nafasi ya saba Jumamosi.

Motta hakuthibitisha kama fowadi Dusan Vlahovic atakuwa tayari kwa pambano hilo.

"Sizungumzi kuhusu soko la uhamisho. Dusan anaendelea kupata nafuu, hayuko katika asilimia 100 na hatuwezi kuhatarisha kumpoteza kwa muda mrefu zaidi, kwa hiyo tutaona kitakachotokea siku tatu zijazo," alisema Motta.

Mfungaji wa mabao wa Juve, Kalulu alikiri kwamba msururu wa matokeo ya sare umeanza kuondoa umakini katika uchezaji wao.

# Kolo Muani anukia kutua Tottenham

**LONDON,** England

PARIS Saint-Germain imepokea ofa ya kwanza kutoka kwa Tottenham Hotspur kwa ajili ya mshambuliaji wa Ufaransa, Randal Kolo Muani, vyanzo vimeiambia ESPN, ingawa klabu hiyo ya Ufaransa imeripotiwa kuwa tayari imefikia makubaliano ya mkopo na Juventus.



Spurs, ambayo ipo nafasi ya 11 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, inatazamia kuimarisha kikosi chao hasa eneo la ushambuliaji na kuwasilisha ofa ya mkopo ikiwa na chaguo la kumnunua.

Hata hivyo, Muani anaweza kutua London kama PSG itashawishika na ofa ya timu hiyo ya Ligi Kuu England na mchezaji mwenyewe ataamua kati ya kujiunga na Spurs au Juventus.

Muani, ambaye ameichezea nchi yake mara 37 akiwa amefunga mabao tisa, anataka kuhamia England na klabu nyingine kama Everton, West Ham United na Aston Villa zimeonesha nia ya kumtaka.

Mshambuliaji uyo mzaliwa wa Paris ameichezea klabu hiyo mechi 14 msimu huu, akifunga mara mbili, lakini anapatikana kwa uhamisho baada ya kuonekana kuwa ni ziada ya mahitaji ya kocha Luis Enrique.

Muani mwenye umri wa miaka 26, hakuwa kwenye kikosi katika mechi mbili zilizopita dhidi ya Saint-Etienne na Monaco na anatarajiwa pia kukosa mechi ya Kombe la Ufaransa dhidi ya Espaly wiki hii, kwa mujibu wa vyanzo vya ESPN.

Sakata la uhamisho ina maana kwamba fowadi huyo anatafuta changamoto mpya miezi 18 tu baada ya kujiunga na klabu yake ya utotoni kwa euro milioni 95 kutoka Eintracht Frankfurt.

## Simba: Tumepata pigo

INATOKA UKURASA 24

"Tukimaliza wa kwanza, robo fainali tutaanzia ugenini, tutamalizia nyumbani, tutakuwa na nafasi nzuri ya kuingia nusu fainali. Kwenye kundi tumezifunga timu mbili na alikuwa bado huyu wa Jumapili, hivyo na yeye anatakiwa apate pumzi ya moto.

Wapinzani wetu CS Constantine wako njiani kuja Tanzania na maofisa wetu wa Simba wako uwanja wa ndege kuwapokea," Ahmed alisema.

Ushindi wowote katika mchezo huo utaifanya Simba kumaliza katika nafasi ya kwanza kwenye kundi lao huku sare ya aina yoyote itawapa uongozi CS Constantine.

Timu hizo zote zimefuzu hatua ya robo fainali, CS Constantine ikiwa na pointi 12 ikifuatiwa Simba yenye pointi 10, Bravos do Maquiz ya Angola iko katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi saba wakati CS Sfaxien ya Tunisia wanaburuza mkia baada ya kufungwa michezo yote mitano.

## Yanga yashtukia 'janja' ya MC Alger

INATOKA UKURASA 24

na mashabiki wa Yanga, wanapaswa kuja uwanjani ili kuwasapoti wachezaji kwa sababu mechi haitakuwa rahisi kama ambayo inafikiriwa. Nafikiri mnaona wanavyofanya ujanja ujanja wanakuja kwa mafungu mafungu. Wamedhamiria kuja kupata pointi tatu au moja, hivyo kila Mwana-Yanga anapaswa kujua kuna jukumu zito la kuujaza uwanja," Kamwe alisema.

Aliwapongeza wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kufuatia mauzo ya tiketi kwenda vyema, hivyo anaamini mpaka Jumamosi angalau mashabiki watafikia idadi ya 50,000 au 60,000 ambayo ndio uwezo wa kujaza uwanja.

"Niwapongeze mashabiki na wanachama, tiketi nyingi tayari zimenunuliwa kabla hata mkutano wa hamasa au klabu kutangaza rasmi uuzwaji wa tiketi, mwamko umekuwa mkubwa sana, wananchi wameonyesha kwa vitendo kwa kiasi gani wanaitaka mechi," Kamwe alisifia.

Kuhusu hali ya wachezaji alisema karibu wote wapo katika hali nzuri, isipokuwa Yao Kouassi huku Maxi Nzengeli akiendelea vizuri.

"Mchezaji wetu Yao atakuwa nje kwa kipindi kisichopungua wiki nne na kisichozidi wiki sita. Maxi anaendelea vizuri na maozezi, kama mwalimu ataona utimamu wake wa kimwili unafaa kucheza, basi mchezo ujao atamtumia lakini kimsingi kwa sasa yupo vizuri," aliongeza.

Yanga na MC Alger zote zinawania nafasi moja, baada ya Al Hilal yenye pointi 10 kufuzu, licha ya kutokuwa na uhakika wa kumaliza ikiwa kinara wa kundi hilo.

Yanga, iko nafasi ya tatu ya msimamo ikiwa na pointi saba, ambapo inahitaji ushindi pekee ili kufuzu, ambapo itafikisha pointi 10 na kuiacha MC Alger ikisalia na pointi nane.

# SERIKALI YAWAANGUKIA WADAU KUELEKEA CHAN, AFCON 2027

**Na Shufaa Lyimo**

SERIKALI imewataka Watanzania kuiunga mkono Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) ili iweze kutwaa ubingwa wa mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), ambayo sasa yatafanyika Agosti, mwaka huu.

Pia serikali imewataka wadau kutoa sapoti kwa timu yao pale itakapochuana katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027), zitakazofanyika Tanzania, Kenya na Uganda.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri Nishati, Doto Biteko, alisema hayo katika kongamano la wadau mbalimbali wa michezo kuelekea maandalizi ya CHAN 2024 pamoja na AFCON 2027.

Biteko alisema ili kufikia malengo, Serikali imejipanga vyema kuhakikisha Taifa Stars inafika mbali katika mashindano hayo kama nchi mwenyeji.

"Serikali imefanya uwekezaji mkubwa kuhakikisha Tanzania inanufaika kupitia mashindano ya CHAN yatakayofanyika mwaka huu, pamoja na yale ya AFCON yatakayofanyika mwaka 2027, yatatumika kuinua uchumi wa nchi yetu," alisema Biteko.

Pia kiongozi huyo alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika sekta ya michezo ambayo imezaa matunda makubwa mpaka nchi yetu kupata fursa ya kuwa wenyeji wa mashindano hayo.

Naye Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma, alisema licha ya mashindano ya CHAN kusogezwa mbele, maandalizi yalikuwa yamekamilika kwa asilimia 99.

"Miezi sita tuliyonayo kwa sasa itatusaidia kufanya maandalizi zaidi yatakayoifanya timu yetu kufanya vizuri, kupitia kongamano hili naamini ushindani utazidi kuwa mkubwa," alisema waziri huyo.

Aliipongeza Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi CHAN na AFCON kutokana na kazi nzuri wanayofanya ili Tanzania ifanye vizuri na kuzidi kuipeperusha vyema bendera ya nchi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, ambaye ni Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema gharama ya kuandaa mashindano kama hayo makubwa ni zaidi ya Sh. trilioni moja.

"Serikali imefanya kazi kubwa kuimarisha miundombinu yote ambayo itatumika katika mashindano hayo mwezi huu, tunatarajia kuongeza viti 20 na vingine vitaletwa ifikapo Machi," alisema Msigwa.

Hata hivyo Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alisema yupo katika mchakato wa kukamilisha miundombinu ya barabara na kuboresha ulinzi ili mpaka ikifika Agosti, mkoa uwe na mvuto mkubwa kwa sababu watakuja wageni kutoka mataifa mbalimbali.

Wilfred Kidao, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), amesema wamefanya maandalizi zaidi ya mwaka mmoja wakiwa na lengo la kuona Tanzania inaweka historia kwa kufika mbali.

"Kutokana na maandalizi tuliyoyafanya tunaamini tutaingia fainali katika mashindano hayo," alisema Kidao.



Wachezaji chipukizi kutoka mikoa mbalimbali nchini wakishiriki katika mazoezi maalumu ya kutambua vipaji yanayoendelea kwenye Kituo cha Ufundi cha Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kilichoko Mnyanjani jijini Tanga jana. **PICHA: TFF**

# Ligi Kuu kurejea mapema

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kuahirisha fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), Bodi ya Ligi, imesema Ligi Kuu Tanzania Bara itarejea mapema.

Awali kufuatia michuano ya CHAN na Kombe la Mapinduzi, bodi hiyo ilitangaza Ligi Kuu Tanzania Bara itasimama hadi Machi Mosi, mwaka huu.

Ofisa Habari wa Bodi ya Ligi, Karim Boimanda, aliliambia gazeti hili sababu zilizopelekea kusogezwa kwa ligi hiyo sasa zote hazipo, hivyo kuna nafasi kubwa ya kurejea mapema baada ya viongozi wanaohusika na usimamizi na uendeshaji wa ligi kukutana.

"Tulitoa taarifa tunafanya hivyo kwa ajili ya kupisha mashindano mawili, Kombe la Mapinduzi na CHAN, moja limeisha lingine limesogezwa mbele na taarifa tumeipata kupitia tovuti yao, bado hatujapokea barua rasmi.

Hatuna sababu tena ya kuendelea kusubiri mpaka siku hizo. Niseme tu taarifa rasmi tutaitoa baada ya idara zote zinazohusika na usimamizi na uendeshaji wa ligi ofisini kukutana, tukimaliza tutatoa taarifa ya kurejea kwa ligi," alisema Ofisa Habari huyo.

Aliongeza kwao hakutakuwa na athari yoyote, na uamuzi huo umewarahisishia kumaliza ligi kwa wakati kwa sababu walikuwa 'wanaumiza kichwa' kuhusiana na muda ambao upo kikanuni.

"Hakutakuwa na kitu hasi, au kutupa tabu sana kwa sababu hata sisi tulikuwa tunaumiza kichwa kama tunaweza kumaliza ligi kwa wakati kutokana na ufinyu wa muda, " Boimanda alisema.

Michezo
Alhamisi Januari 16, 2025
Nipashe



Kolo Muani anukia kutua Tottenham UKURASA 22

# Yanga yashtukia 'janja' ya MC Alger



Wanachama na mashabiki wa Yanga kutoka sehemu mbalimbali jijini Dar es Salaam wakishiriki maandamano kama sehemu ya hamasa ili kujitokeza kwa wingi keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kushuhudia mechi ya raundi ya sita ya Kundi A ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya MC Alger kutoka Algeria. **PICHA: MTANDAO**

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema msafara wa wachezaji na viongozi wa MC Alger kutoka Algeria uliotarajiwa kuwasili nchini jana alfajiri haujaonekana, hivyo hali hiyo imewataka kuongeza umakini kuelekea mchezo utakaofanyika keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, imeelezwa.

Yanga itawakaribisha MC Alger katika mechi ya raundi ya sita ya Kundi A utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ambapo wenyeji wanahitaji ushindi wa aina yoyote ili kufuzu hatua ya robo fainali.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema taarifa kutoka kwa uongozi wa MC Alger zilieleza walitarajia kuwasili nchini jana alfajiri lakini ugeni huo haujaonekana na badala yake wamalishuhudia ujio wa mashabiki na baadhi ya maofisa wa timu hiyo wakiwasili kwa 'mafungu'.

Kamwe alisema hii yote haifanyiki kwa bahati mbaya, badala yake ni mpango mkakati na unaoratibiwa na wapinzani wao kwa ajili ya kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo huo.

"Taarifa ambazo tunazo wapinzani wetu walipaswa kuingia nchini alfajiri ya kuamkia leo (jana), lakini mpaka sasa hatujawaona na sisi kama klabu tulifanya wajibu wetu lakini hawakutokea, tukipata taarifa rasmi basi tutawajuza. Kimsingi tunahitaji kuwaona uwanjani Jumamosi mengine hayatuhusu," alisema Kamwe.

Aliongeza kwa mabadiliko hayo yanawapa 'picha' kubaini wapinzani wao pia wamedhamiria mapambano ya kusaka ushindi au sare ili wasonge mbele.

"Niwaambie tu wanachama

INAENDELEA UK. 23

# Simba: Tumepata pigo

## ●●● Ni adhabu ya kucheza bila mashabiki Jumapili, yawatoa hofu...

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) kutoa adhabu kwa Simba kucheza bila mashabiki katika mechi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya CS Costantine kutoka Algeria, Kocha wa timu hiyo, Fadlu Davids, amesema hilo ni pigo kwa Wekundu wa Msimbazi.

Simba itaikaribisha CS Constantine katika mechi ya mwisho ya Kundi A itakayochezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

CAF pia imeipiga Simba faini ya Dola za Marekani 40,000 kufuatia vurugu za mashabiki wake katika mechi dhidi ya CS Sfaxien ambayo ilichezwa hapa nchini na wenyeji kupata ushindi wa mabao 2-1.

CS Sfaxien pia wamepigwa faini ya Dola za Marekani 40,000 kutokana na wachezaji, viongozi na mashabiki wake kufanya vuguru katika mchezo huo, CAF wametoa siku 60 za kulipa faini hiyo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Fadlu alisema mashabiki ni muhimu katika mchezo huo wa kusaka nafasi ya kuongoza kundi lao lakini 'hakuna namna' ya kuikwepa adhabu waliyopewa.



Fadlu alisema wamejiandaa kupambana ili kusaka ushindi na hatimaye kumaliza hatua hiyo ya makundi wakiwa kileleni baada ya timu zote mbili tayari zimeshatinga robo fainali ya michuano hiyo.

"Muhimu zaidi kwetu ni kuhakikisha tunashinda na kupata pointi tatu, najua mashabiki ni muhimu sana, lakini ni lazima tupambane ili tushinde hata kama mashabiki wetu hawatakuwepo, huko watakapokuwepo watatuombea.

Jukumu la kwanza la kuingia robo fainali limefanikiwa, sasa hivi tunahitaji ushindi ili kumaliza kwa heshima, linaweza hata kama hatutakuwa na mashabiki wetu, tutapambana kwa dakika zote, tunataka kumaliza katika nafasi ya kwanza kwenye kundi letu," alisema Fadlu.

Kocha huyo alisema wachezaji wake wameonyesha wana na morali na mchezo huo ambao wanataka kulipiza kisasi cha kufungwa katika mchezo wa kwanza waliocheza ugenini ambao walipoteza kwa mabao 2-1.

"Mchezo huu kila mchezaji ana ari na morali kubwa, tunataka kwanza kulipiza kisasi cha kufungwa mchezo wa kwanza, lakini lengo kuu kupata pointi tatu tuweze kuongoza kundi letu," Fadlu alisema.

Nahodha wa Simba, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr', alisema wanaendelea na maandalizi yao huku wakifuata kile wanachoambiwa na kocha wao kuelekea katika mchezo huo.

"Sisi tupo vizuri, tunaendelea na maandalizi yetu, kila mchezaji yupo vizuri na yupo tayari kwa mchezo huu, tunaamini tutawapa furaha mashabiki wetu ambao hawatakuwepo uwanjani," alisema beki huyo.

Wakati huo huo, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, kikosi chao kiliingia kambini jana kwa ajili ya kujiandaa na mchezo huo.

Ahmed alisema wataingia katika mechi hiyo kwa lengo moja la kusaka pointi tatu ili kuwarahisishia kuanzia ugenini kwenye hatua ya robo fainali.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002